# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# RIPOTI YA KAMATI YA KANUNI NA SHERIA NDOGO NDOGO KUHUSU UCHAMBUZI WA KANUNI NA SHERIA NDOGO NDOGO ZILIZOWASILISHWA MEZANI NA SERIKALI KWAMWAKA 2022

February, 2023.

## YALIYOMO

**Sehemu ya Kwanza**

**Utangulizi**

Maelezo ya Utangulizi........................................4

Mamlaka ya Kutunga Sheria........................................5

Udhibiti wa Utungaji wa Kanuni na Sheria Ndogo ndogo........................................5

Utekelezaji Majukumu ya Kamati........................................7

Uwasilishwaji Mezani wa Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo Katika Mwaka 2021....................8

Kufanya Uchambuzi wa Kanuni na Sheria Ndogo ndogo yoyote ambayo inatumika......................9

Kanuni Zilizowasilishwa 2022........................................10

**Sehemu ya Pili**

**Mapungufu Mbalimbali ya Sheria**

Sheria ya Tafsiri........................................13

Sheria ya Tawala za Mikoa........................................15

Sheria ya Shirika la Bandari........................................16

Sheria ya Mahakama ya Kadhi........................................17

**Sehemu ya Tatu**

**Uchambuzi wa Kanuni**

Maudhui ya Jumla........................................19

Ukiukwaji wa Sheria........................................20

Matumizi ya Lugha........................................22

Makosa ya Kisarufi........................................23

**Sehemu ya Nne**

**Ziara za Kamati**

Shirika la Utangazaji, Zanzibar (Dar es Salam)........................................24

Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF)........................................26

Mamlaka ya Bandari Tanzania........................................27

Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania....................................................................................29
Kampuni ya Uendeshaji Uwanja wa Ndege Kilimanjaro (KADCO)................................................31

**Sehemu ya Tano**

Mapendekezo ya Kamati......................................................................................................33
Hoja za Kamati....................................................................................................................35

**Sehemu ya Sita**

Hitimisho...........................................................................................................................36
Viambatanisho....................................................................................................................39
Kiambatanisho Namba 1......................................................................................................40
Kiambatanisho Namba 2......................................................................................................48
Kiambatanisho Namba 3......................................................................................................56
Kiambatanisho Namba 4......................................................................................................65
Kiambatanisho Namba 5......................................................................................................72

## SEHEMU YA KWANZA

## MAELEZO YA UTANGULIZI

### 1. Utangulizi

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote tumshukuru Allah Mwingi wa rehma na mwenye kurehemu, ambae kwa utukufu wake ametuwezesha sisi kuwa ni miongoni mwa wawakilishi wa wananchi wa Zanzibar. Ni wajubu wetu kutekeleza kwa weledi na kwa uaminifu mkubwa ili kuleta chachu ya maendeleo kwa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla.

Aidha, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo ndogo, naomba nikushukuru wewe binafsi kwa kutupa heshima kubwa na kutuamini katika jukumu zito la kupitia na kuchambua kanuni mbalimbali za ndani ya visiwa vyetu. Nikushukuru pia kwa kutoa idhini kwa Kamati yangu iweze kuwasilisha Ripoti ya uchambuzi wa kanuni zilizowasilishwa Mezani na Serikali mwaka 2022 na zile ambazo Kamati kwa kuona umuhimu wake iliziita kwa ajili ya kufanyiwa uchambuzi wa kisheria.

**Mheshimiwa Spika,** natumaini kuwa ripoti hii itawezesha Waheshimiwa Wawakilishi kutoa ushauri zaidi kuhusu Kanuni na Sheria Ndogo ndogo zilizochambuliwa na Kamati pamoja na Kanuni nyingine ambazo zinatumika. Pia, Kamati inaamini kuwa Serikali itayafanyia kazi mapendekezo yaliyomo katika Taarifa hii na maoni yatakayotolewa na Wawakilishi ili kuondoa dosari zilizobainika kutokana na uchambuzi wa Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** ripoti hii ya kamati ya Kanuni na Sheria ndogo ndogo imegawika katika sehemu kuu tano (5) nazo Maelezo ya Utangulizi, Maoni ya Jumla, Uchambuzi wa Kanuni mbalimbali, Mapendekezo ya Kamati na mwisho ni Viambatanisho.

### 1.2 Mamlaka ya Kutunga Sheria

**Mheshimiwa Spika,** Ibara ya 78 ya Katiba ya Zanzibar, 1984, imeipa Baraza la Wawakilishi mamlaka yote ya kutunga Sheria juu ya mambo yote ya yasiyo ya Muungano yahusuyo Zanzibar,

> "*Nguvu za kutunga sheria kwa mambo yote yasiyokuwa ya Muunganokatika Zanzibar yatakuwa mikononi mwa Baraza la Wawakilishi"*

Aidha, Ibara ya 78(2) ya Katiba imeweka utaratibu ambao unapaswa kuzingatiwa na Baraza la Wawakilishi katika kutekeleza madaraka yake ya kutunga Sheria.

> *"Bila ya kuathiri masharti mengine ya Katiba hii, nguvu za kutunga sheria katika Baraza la Wawakilishi itakuwa kwa kupitishwa Miswada katika Baraza la Wawakilishi."*

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mamlaka hayo, Baraza la Wawakilishi kwa mujibu wa Ibara ya 79(6) cha Katiba ya Zanzibar, 1984 limekasimu madaraka yake ya kutunga Sheria kwa mtu yeyote au idara yoyote ya Serikali kutunga sheria Ndogo ndogo *(subsidiary legislation/delegated legislation)* ambazo hujumuisha Kanuni mbalimbali *(rules and regulations)* pamoja na Sheria Ndogo ndogo za Serikali za Mitaa *(By-Laws)* kama zinavyotafsiriwa chini ya Sheria ya Tafsiri ya Sheria Nam. 7 ya Mwaka 1984.

### 1.3 Udhibiti wa Utungaji wa Kanuni na Sheria Ndogo ndogo

**Mheshimiwa Spika,** Udhibiti wa utungaji wa Kanuni na Sheria Ndogo ndogo hubaki katika mikono ya Baraza la Wawakilishi *(House Control Over Subsidiary Legislation.* Utaratibu huu ni wa kawaida katika Mabunge ya nchi za Jumuiya ya Madola ambao unalenga kuliwezesha Baraza la Wawakilishi kujiridhisha juu ya matumizi ya mamlaka hayo ya kutunga sheria lililoyakasimu kwa mamlaka nyingine.

**Mheshimiwa Spika,** utaratibu huu umezungumziwa na waandishi wengi wakiwemo Jain and Jain katika kitabu chao kiitwacho The *Principles of Administrative law* (2007) ukurasa wa 175 wanaposema;

Naomba kunukuu kwa tafsiri isiyo rasmi;

> *"…….kwa kuwa Baraza la Wawakilishi limetoa madaraka ya utungaji sheria kwa vyombo vingine, wajibu wake mkubwa ni kuhakikisha kunakuwepo matumizi sahihi ya madaraka yaliyo kasimiwa ya kutunga sheria, kusimamia na kudhibiti matumizi ya mamlaka hayo ili kuondoa uwezekano wa vyombo hivyo kutumia vibaya madaraka yaliyokasimiwa.."*
>
> ***Mwisho wa kunukuu***

**Mheshimiwa Spika,** kwa maelezo hayo utaratibu wa kuchambua Kanuni na kutoa Taarifa ndani ya Baraza kunaliwezesha Baraza la Wawakilishi kujiridhisha na namna madaraka yake yaliyo kasimiwa kwa Taasisi za Serikali yanavyotumika.

**Mheshimiwa Spika,** suala la udhibiti wa Kanuni na Sheria Ndogo ndogo pia limewekwa katika Sheria ya Tafsiri ya Sheria, *(The Interpretation of Laws Act,)* ambayo imeweka masharti maalum yanayolipa Baraza la Wawakilishi mamlaka ya udhibiti wa Kanuni na Sheria Ndogo ndogo zinazotungwa na Serikali pamoja na vyombo vyake. Hata hivyo udhibiti huo siyo wa moja kwa moja kwa sababu Baraza la Wawakilishi halina mamlaka ya kuingilia mchakato wa kutungwa kwa Kanuni yoyote mpaka Kanuni na Sheria Ndogo ndogo hizo zinapotangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali na kuwasilishwa Barazani.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na umuhimu wa kufanya Udhibiti wa Utungaji wa Kanuni na Sheria Ndogo ndogo, Kanuni ya 107 ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi Toleo la 2020 ikisomwa kwa pamoja na Jadueli la kwanza la Kanuni hizi, imeanzisha majukumu ya Kamati hii kama ilivyo kwa Mabunge mengine katika Nchi za Jumuiya ya Madola. Miongoni mwa majukumu yake ni;

a. kufuatailia utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa kwenye repotiya Kamati ya Mwaka;

b. kuchambua Kanuni na Sheria Ndogo ndogo ili kujiridhisha iwapo zimekidhi matakwa ya masharti ya Katiba, Sheria Mama na sheria nyengine;

c. kujadili na kutoa mapendekezo kwa taasisi husika juu ya namna bora ya kutengeza kanuni na sheria ndogo ndogo;

d. kulishauri Baraza kubatilisha Kanuni na Sheria Ndogo ndogo ambazo zinakiuka masharti ya Katiba, masharti ya Sheria Mama au sheria nyenginezo za nchi;

e. kufikiria jambo jengine lolote litakalopelekwa kwake na Spika

### 1.4 Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika,** wajibu wa msingi wa Kamati kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, kama ambavyo imeelezwa awali, ni kufanya uchambuzi wa Kanuni na Sheria Ndogo ndogo ili kujiridhisha iwapo zimekidhi matakwa na masharti ya Katiba, Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi.

Aidha, Kanuni na Sheria Ndogo ndogo hutungwa kwa lengo la kuwezesha utekelezaji wa Sheria Mama katika masuala mbalimbali. Kanuni na Sheria Ndogo ndogo zinajumuisha:-

*1.* Amri*(Orders)*
*2.* Matamko *(Proclamations)*
*3.* Kanuni za Taasisi *(Rules)*
*4.* Kanuni za Mahakama *(Rules of Court)*
*5.* Kanuni za Wizara *(Regulations)*
*6.* Taarifa*(Notices)*

7. Kanuni na Sheria Ndogo ndogo za Halmashauri (*By – Laws)*

8. Hati *(Instruments)*

## 2.0 Uwasilishwaji wa Kanuni na Sheria Ndogo ndogo katika Mwaka 2022

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni zetu za Baraza zimeweka sharti la kuletwa Barazani Kanuni au Sheria ndogondogo iliyotungwa na mamlaka nyingine nje ya Baraza la Wawakilishi baada ya kutangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali. Aidha, Kanuni pia zimetoa fursa kwa Kamati kuitisha Kanuni yoyote kwa minajili ya kuipitia. Baada ya Baraza la Wawakilishi kupokea Kanuni hizo, Kamati hufanya uchambuzi wake na baadae kutoa maoni na ushauri kuhusu yaliyomo katika Kanuni husika. Katika kutekeleza hayo Kanuni zetu za Baraza zimeainisha hatua zinazoweza kuchukuliwa na Baraza la Wawakilishi. Hatua hizo ni:-

### *i)* Kutoa Azimio la kuzuia kutumika kwa Kanuni au Sheria Ndogo husika *(disallowance resolution)*

Kanuni inaruhusu Baraza la Wawakilishi kupitisha Azimio la kuzuia kutumika kwa Kanuni au Sheria Ndogo endapo litajiridhisha na maoni ya Kamati kwamba, Kanuni haikidhi masharti na matakwa ya Katiba, Sheria Mama au Sheria nyingine ya nchi.

### *ii)* Kufanya marekebisho au kubadili Kanuni au Sheria Ndogo yoyote kufuatia Azimio la kuzuia kutumika kupitishwa na Baraza la Wawakilishi *(amendment and substitution)*

Katika kutekeleleza mamlaka yake yaliyoainishwa katika aya ya (i), Baraza la Wawakilishi linaweza kupitisha Azimio muda wowote ili kurekebisha au kubadili Kanuni au Sheria Ndogo yoyote iliyozuiwa kutumika.

## 2.1 Kufanya Uchambuzi wa Kanuni na Sheria Ndogo ndogo yoyote ambayo inatumika

**Mheshimiwa Spika,** kwa madhumuni ya utekelezaji mpana wa Kanuni ya 107 ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi toleo la 2020, Kamati inaweza kufanya uchambuzi wa Kanuni na Sheria Ndogo ndogo yoyote kwa kuzingatia vipaumbele inavyojiwekea.

**Mheshimiwa Spika,** kwa madhumuni ya kuliwezesha Baraza lako tukufu kufuatilia ipasavyo utekelezaji wa madaraka yake ya kutunga sheria yaliyokasimiwa kwa mamlaka mbalimbali, naomba kubainisha mambo ambayo yanayozingatiwa na Kamati wakati wa uchambuzi wa Kanuni na Sheria Ndogo ndogo zilizowekwa Mezani. Mambo hayo ni:-

a) Iwapo Kanuni na Sheria Ndogo ndogo husika inakiuka Katiba ya Zanzibar, 1984;
b) Iwapo Kanuni na Sheria Ndogo ndogo husika inavuka mipaka au kwenda kinyume na masharti ya Sheria inayotoa mamlaka ya kutunga Kanuni na Sheria Ndogo hizo au Sheria nyingine yoyote;
c) Iwapo Kanuni au Sheria Ndogo husika imezingatia misingi bora ya uandishi wa Sheria *(drafting principles)*;
d) Iwapo Kanuni au Sheria Ndogo husika inakiuka misingi ya haki za binadamu;
e) Iwapo Kanuni na Sheria Ndogo ndogo inatekelezeka kwa urahisi kiuchumi na kijamii,na
f) Makosa ya uandishi na uchapaji.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kukamilisha uchambuzi wake kwa kuzingatia masuala yaliyotajwa, Kamati hubaini hoja mbalimbali zinazolenga kupata ufafanuzi katika maeneo ya Kanuni na Sheria Ndogo ndogo zenye dosari. Hoja hizo huwasilishwa Serikalini kwa lengo la kupendekeza marekebisho au kufutwa kwa kifungu chochote ambacho kina dosari zilizobainishwa na Kamati. Kila Wizara inayoguswa na hoja zinazoibuliwa na Kamati, huwajibika kufika mbele ya Kamati na kutoa maelezo

kuhusiana na Kanuni yake.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo napenda nilijulishe Baraza lako Tukufu kuwa Taarifa hii inahusisha uchambuzi wa Kanuni na Sheria Ndogo ndogo zilizowasilishwa katika Mikutano ya Baraza la Wawakilishi kwa mwaka 2022

## 3.0 KANUNI NA SHERIA NDOGO NDOGO ZILIZOWASILISHWA 2022

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka 2021 Serikali iliwasilisha Mezani Kanuni na Sheria Ndogo ndogo Ishirini na Tatu (23) Kanuni na Sheria Ndogo ndogo hizo ziligawanyika katika mchanganuo ufuatao:-

a) Kanuni za Wizara (*Regulations*) 20

b) Amri (*Orders*) 1

c) Kanuni na Sheria Ndogo ndogo za Halmashauri (*By – Laws*) 2

**Mheshimiwa Spika,** katika kutilia nguvu masharti ya Kanuni ya 25 ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi ambayo imeelekeza kuwa majadiliano ndani ya Baraza yatafanyika kwa lugha ya Kiswahili, hivyo, Kanuni 12 ambazo ziliandikwa kwa lugha ya Kiingereza na kuwasilishwa bila ya muambatano wa Kanuni au Sheria ndogo iliyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili zilirejeshwa kwa Taasisi husika. Kwa minajili ya kuwasaidia wananchi ambao ndio watumiaji au walengwa wakuu wa Kanuni hizo, Kamati ilitoa agizo kwa Taasisi hizo kuandika upya Kanuni na Sheria ndogo hizo kwa lugha ya Kiswahili na kuziwasilisha tena Barazani.

**Mheshimiwa Spika**, Kanuni zilizorejeshwa ni kama ifuatavyo:-

1. The Value Added Tax, (Amendment of Schedules) Order, 2022
2. The Zanzibar Food, Drugs and Cosmetics (Registration of Premises, importation and

Exportation of Pharmaceutical Products and Raw Materials) Regulations, 2022

3. The Medical and Dental Practitioners Registration and Licensing Regulations, 2019
4. The Business Licensing Administration (Amendment) Regulations, 2022
5. The Fees and Charges (Upstream) Regulations, 2022
6. The Health, Safety and Environment (Upstream) Regulations, 2022
7. The Anti-Money Laundering and Proceeds of Crime Regulations, 2022
8. The Zanzibar Bureau of Standards (Fees and Charges) Regulations, 2022
9. The Law School of Zanzibar (Admission, Fees and Conduct of Practical Legal Training) Regulations, 2021
10. The Student Code of Conduct Regulations, 2021
11. The Import and Export of Precious Metals and Precious Stones Regulations, 2022

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni zilizochapishwa kwa lugha ya kiswahili na kuwasilishwa Barazani kwa mwaka 2021 ni kama ifuatavyo;

1. Kanuni za Usafi na Adhabu za Papo kwa Papo, 2021
2. Kanuni za Mwenendo wa Mahakama ya Kadhi, 2021
3. Kanuni za Utumishi za Shirika ZBC, 2021
4. Kanuni za Utendaji kwa Watoa Msaada wa Kisheria, 2021
5. Kanuni za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar, 2007 (pamoja na marekebisho ya 2017)
6. Kanuni za Utumishi za Shirika la Bima Zanzibar, 2017
7. Kanuni za Utumishi za Benki ya Watu wa Zanzibar, 2022
8. Kanuni za Utumishi za Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, 2016
9. Kanuni za Taasisi ya Viwango Zanzibar (Ada na Tozo), 2022
10. Kanuni za Ushuru wa Huduma za Baraza la Manispaa Mjini, 2022

**11.** Kanuni za Tozo za Huduma na Biashara za Baraza, 2022

**12.** Kanuni za Utumishi za Shirika la Bandari Zanzibar, 2012

## 2. Sehemu ya Pili

### Maoni ya Jumla ya Kamati

**Mheshimiwa Spika,** katika kupitia na kuchambua Kanuni mbalimbali kama zilivyoainishwa katika sehemu iliyopita, Kamati imekumbana na changamoto mbali zisizohusiana na utungwaji wa kanuni zilizoainishwa ila ni zile changamoto ambazo zinapelekea kuzorota kwa utelekezwaji wa Sheria na Kanuni mbalimbali katika nchi yetu. Changamoto hizo kama hazitafanyiwa utaratibu wa haraka utazorotesha upatikanaji wa maendeleo chanya yanayoendana na matakwa ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na sera za Chama cha Mapinduzi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa minajili ya ripoti hii inayowasilishwa kwako na Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo ya Baraza hili Tukufu, changamoto ambazo zinakwaza utungaji na utekelezwaji wa Kanuni mbalimbali ni kama ifuatavyo:

2.1 **Mapungufu ya Sheria Mbalimbali**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati katika uchambuzi wa kupitia Kanuni mbalimbali imeridhishwa na nia njema ya Serikali katika kutunga na kuzifanyia marekebisho kanuni na sheria ndogondogo ambazo zinaonekana kutokwenda na wakati kwa lengo la kuboresha utekelezaji bora wa sheria husika. Hata hivyo, Kamati katika uchambuzi huo ulibaini mapungufu ya Sheria mbalimbali ikiwemo Sheria ya Tafsiri (Sheria namba 7 ya 1984), Sheria ya Tawala za Mikoa, 2014 Sheria ya Bandari na nyenginezo.

**2.1.a Sheria ya Tafsiri No. 7 ya 1984**

**Mheshimiwa Spika,** Katika ripoti ya Kamati hii ya 2022 iliyowasilishwa katika Baraza hili tuliielekeza Serikali kufanya mchakato wa kufanyia marekebisho Sheria namba 7 ya 1984 ambayo kimsingi haiendani na wakati uliopo sasa na kuwa kipingamizi cha utekelezaji wa kanuni mbalimbali katika

visiwa vyetu. Aidha, katika ripoti yetu tulibainisha maeneo ambayo Sheria hii imekuwa ni kikwazo kwa kanuni mbalimbali hususan Kifungu cha 42(e) cha Sheria hii ambayo imetaka faini zozote zitakazoainishwa katika Kanuni au sheria ndogo zisizidi zaidi ya Shilingi za Kitanzania Elfu Saba (Tsh. 7,000) au kifungo kisichozidi miaka miwili (2)

**Mheshimiwa Spika,** kwa muktadha huo takriban Kanuni zote zilizopo katika nchi yetu faini zake ni zaidi ya kiwango kilichoainishwa katika kifungu hicho, hivyo pale anapotokea mjuvi wa fani ya sheria zinaweza kupingwa mbele ya Mahakama kuwa zinakiuka matakwa ya sheria za nchi.

**Mheshimiwa Spika,** Sheria za tafasiri katika nchi za Jumuia ya Madola hulenga kuondoa utata unaojitokeza katika tafasiri ya sheria mbalimbali zinazotungwa na mamlaka ya nchi husika, ila kwa sheria ambayo sisi tupo nayo yenyewe inatoa mwanya kwa Mahakama au taasisi mbalimbali kuwa na tafasiri mbadala pale inapotokea mkwamo wa kisheria. Kifungu cha 42 cha Sheria hiyo ya tafasiri imeainisha mamlaka ambazo zimeanzishwa na kupewa uwezo kwa mujibu wa sheria kutunga kanuni na sheria ndogondogo, ila kutokana na mahitaji ya Serikali baadhi ya Taasisi zinashindwa kujua nafasi yao kwa mujibu wa kifungu hiki cha sheria. Mfano wa taasisi hizo ni kama Benki ya Watu wa Zanzibar ambayo ilianzishwa kwa kusajiliwa chini ya sheria ya makampuni ya Zanzibar (The Companies Act, 2012). Utata ambao uliwahi kuibuka katika baadhi ya mashauri yaliyowasilishwa Mahakamani dhini ya Benki hiyo ni kuwa je Bodi ya Benki ya Watu wa Zanzibar ambapo kwa mtazamo wa juu imeakisi matakwa ya Sheria ya Hazina *(The Treassurer Act)* ina mamlaka ya kutunga kanuni na kuchapishwa katika gazzeti rasmi?. Mheshimiwa Spika, jibu linakosekana kwa sababu ya kukosekana muangaza ndani ya sheria namba 7 ya 1984.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na mapungufu ya sheria hii ya tafasiri namba 7 ya 1984, ni maoni ya Kamati kuwa, Baraza lako Tukufu kupitisha azimio la kuitaka serikali kuanza mchakato wa kuifanyia marekebisho heria hiyo ipasavyo kuhusu namna bora ya kuboresha baadhi ya maudhui yanayoendana na

wakati huu, ili kuleta ufanisi wa utekelezaji wa sheria na kanuni mbalimbali.

2.1.b. **Sheria ya Tawala za Mikoa, No 7 ya 2014**

**Mheshimiwa Spika,** baadhi ya vifungu vya sheria hii vinakwaza utendaji wa kimamlaka kwa Mabaraza ya Jiji, Manispaa, halmashauri na miji. Kifungu cha 12 cha sheria hii, kimekasimu mamlaka ya Serikali kuu kwa mujibu wa kiambatanisho cha kwanza cha sheria husika kwa mabaraza ya Jiji, Manispaa, halmashauri na miji. Kifungu hiko pia kimekipa uwezo mamlaka za juu katika serikali za mitaa kukasimu baadhi ya mamlaka yao kwa mabaraza ya chini yao. Hata hivyo, sheria hii haikuweka mgawanyo wa madaraka yaliyoainishwa katika kiambatanisho cha kwanza kati ya Mabaraza hayo.

**Mheshimiwa Spika,** kukosekana kwa mgawanyo na ukomo wa kimamlaka katika sheria ya Tawala za Mikoa kunapelekea mgongano mkubwa wa kiutendaji kati ya Jiji na Manispaa hususan Manispaa ya Mjini. Kiambatanisho cha kwanza katika sheria hiyo kimetoa mamlaka kwa mabaraza kuandaa mkakati wa vyanzo vya mapato ndani ya maeneo yao kwa kuweka utaratibu wa kisheria wa kukusanya mapato hayo. Hata hivyo uanzishwaji wa Baraza la Jiji haukuangalia kiuhalisia utekelezwaji wa matakwa hayo ya sheria. Aidha Mabaraza ya Manispaa yamekua yakitunga Kanuni mbalimbali zenye lengo la kutoa huduma na kukusanya mapato ndani ya maeneo yao ambayo pia kisheria yanahudumiwa na Jiji. Kukosekana kwa mgawanyo na ukomo wa kimamlaka kumepelekea Jiji kukosa shughuli za kufanya katika kujipatia mapato. Kadhia hii, huathiri pia shughuli za watu wanaoishi katika maeneo hao kwani mamlaka mbili tofauti hulazimisha kutekeleza wajibu mmoja kwa wakati mmoja. Mfano wa maeneo yenye mgongano ni mamlaka ya kukamata wanyama wanaotembea barabarani, kodi mbalimbali kwa mujibu wa sheria hii na huduma zilizokasimiwa kwa serikali za mitaa.

**Mheshimiwa Spika,** kukosekana kwa ukomo wa uwezo wa ukusanyaji wa mapato kwa Mabaraza, yanapelekea taasisi hizo kutunga kanuni na sheria ndogo zinazokwenda kinyume na utaratibu wa sheria nyengine. Mfano wa kanuni hizo ni **Kanuni ya Ushuru ya Baraza la Manispaa ya Mjini, 2022**

ambayo ililenga kukusanya ushuru wa asilimia tatu (3%) kwa mwaka wa fedha kwa bidhaa na huduma zinazalishwa na kutolewa katika maeneo hayo. Aidha kanuni hiyo pia imelazimisha wawekezaji na wafanyabiashara kuwasilisha hesabu za mapato yao kila mwaka na kuweka adhabu kwa atakaekaidi amri hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** mamlaka ya ukusanyaji wa kodi kwa maana ya *Tax* na ushuru kwa maana ya *Customs Duty* kwa bidhaa zinazozalishwa nchini au huduma zinazotolewa upo chini ya mamlaka ya Serikali kuu na sio Serikali za Mitaa. Kwa upande wa Zanzibar sheria kuu zinazoratibu ukusanywaji wa kodi na ushuru ni **Sheria ya Mamlaka ya Mapato Zanzibar, Nam. 11 ya 2022** pamoja na Sheria za **Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).** Kamati ilihoji sana ya kuwa ni wapi ambapo Manispaa ya Mjini ilipata mamlaka ya kutunga kanuni za kukusanya ushuru wa bidhaa zinazozalishwa katika maeneo yao na huduma zinazotolewa.

2.1.c **Sheria ya Shirika la Bandari la Zanzibar, Nam. 1 ya 1997**

**Mheshimiwa Spika,** sheria hii ilitungwa kwa madhumuni ya kuanzisha Shirika la Bandari Zanzibar pamoja na mamlaka yake kisheria na ya kiutendaji. Hata hivyo sheria hii imekuwa na mapungufu mengi yanayokwamisha utekelezwaji wa Kanuni mbalimbali zilizotungwa chini ya sheria hii. Sheria hii imetambua uwepo wa wafanyakazi wa kada mbalimbali pamoja na maslahi yao, hata hivyo kundi kubwa la wafanyakazi wa Bandari katika kada za chini kama makuli na wasafishaji halikuainishwa katika sheria hiyo. Mapungufu hayo ya kisheria yamepelekea hata kanuni zilizotungwa kutokidhi uhalisia wa kiuendeshaji wa bandari na kusababisha mgogoro mkubwa ndani ya shirika kati ya uongozi na wafanyakazi wa kundi C.

**Mheshimiwa Spika,** uundwaji wa shirika unalenga kutengeneza faida kwa Serikali, hata hivyo, sheria hii haikuweka mazingira ya uwekezaji katika uendeshaji wa bandari mbalimbali katika visiwa vyetu vya

Zanzibar. Kwa hali ya sasa shirika linahitaji wawekezaji ili kupanua shughuli zake hata hivyo, mapungufu haya ya kisheria yanalibana shirika kutunga kanuni mbadala zitakaweka utaratibu wa ubia kati ya shirika na muwekezaji.

**Mheshimiwa Spika,** hizo ni baadhi tu ya sheria ambazo Kamati hii imeona haja ya kulitanabahisha Baraza lako na Serikali kwa ujumla. Kwa muktadha huu tunaliomba Baraza lako tukufu kutoa azimio la kuitaka Serikali kufanya mapitio ya sheria mbalimbali zilizopitwa na wakati na zile zinazokwaza utekelezaji mzuri wa taasisi husika. Mapitio hayo yatawezesha Baraza kufuta na kutunga sheria mpya pamoja na kuzifanyia marekebisho sheria nyenginezo kwa mujibu wa mahitaji ya Zanzibar.

**2.1.d Sheria ya Mahakama ya Kadhi, Nam 9 ya 2017**

Sheria hii namba 9 ya mwaka 2017 iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi, Zanzibar ililenga kuanzisha Mahakama ya Kadhi na mamlaka yake katika kutatua mashauri yote ya Kiislamu yanayohusu ndoa, talaka, mirathi, usimamizi wa watoto na kadhalika. Sheria hii imeweka utaratibu wa kiislamu wa uendeshaji wa mashauri pamoja na kuchanganya utaratibu ulioainishwa katika Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Madai *(Cap 8 of the laws of Zanzibar)* na Sheria ya Ushahidi, nam.9 ya 2016. Hata hivyo, kutokana na mapungufu ya sheria hii ikiwemo uwekaji wa ukomo wa mamlaka *(jurisdiction),* vigezo vya maulamaa, mamlaka ya wasuluhishi pamoja na mahitaji *(reqirements)* ya uanzishwaji wa mahakama hizi, kumepelekea ugumu katika utekelezwaji matakwa ya Kanuni iliyotungwa chini ya sheria hii na kupelekea baadhi ya kanuni kuzalisha jambo ambalo sheria ipo kimya.

**2.2 Mazingira ya utungaji wa Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo**

**Mheshimiwa Spika,** kwa kawaida utungaji wa sheria yoyote ili huanza kwa utafiti wa kina kwa yale maudhui yanayohitajika kutungiwa sheria, na baada ya utafiti huo kuchakatwa vyema, maoni ya wadau ambao ndio watumizi wa sheria hiyo huchukuliwa katika kuiboresha zaidi. Hatua hizi ni muhimu sana

kupitiwa katika utungaji wa sheria yoyote iwe ni sheria kuu, kanuni ama sheria ndogo ndogo. Hata hivyo kukosekana kwa hatua hizi kunapelekea kuwepo kwa mapungufu na kutokutekelezeka kwa sheria hizo.

**Mheshimiwa Spika,** kamati katika kupitia kanuni mbalimbali imegundua kuwa kuna baadhi ya watendaji waliopo kwenye taasisi mbalimbali za Serikali kutokufuata misingi ya uandishi wa Kanuni wanazohusika nazo kutokana na uelewa mdogo wa masuala ya uandishi wa sheria, kutokushirikisha wadau ipasavyo, au uharaka wa kazi waliyonayo.

**Mheshimiwa Spika,** kukosekana kwa utafiti wa kina husababisha kutungwa kwa Kanuni isiyoendana na matakwa ya sheria husika. Mfano, **Kanuni ya Ushuru ya Baraza la Manispaa ya Mjini, 2022.** Kanuni hii ilikosa utafiti wa kina wa kisheria kwa kuipa Manispaa mamlaka ya kukusanya ushuru wa bidhaa zinazozalishwa ndani ya Manispaa, kazi ambayo sheria za kodi Zanzibar imetoa mamlaka hayo kwa Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA). Hivyo, kuiruhusu kanuni hii ni kwenda kinyume na sheria ya tawala za mikoa pamoja na sheria ya mamlaka. Kwa lugha nyengine kanuni hii ni *ultra vires.*

## Sehemu Tatu

## Uchambuzi wa Kanuni

### 3.1 Maudhui ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya uchambuzi kwa kupitia Kanuni kumi na mbili (12) ambapo Kamati imeridhishwa na nia njema ya Serikali kuhusu kutunga Kanuni hizi kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa sheria mbalimbali kama zinavyoelekeza. Hata hivyo, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina na kubaini masuala mahsusi Mawili(2) ambayo ndiyo yaliyoibua mjadala baina ya Kamati, Wadau na Serikali. Mambo hayo ni pamoja na masuala ya kiuandishi wa Mantiki kwenye baadhi ya vifungu vya Kanuni hizi, ambapo kwa mtazamo wa Kamati kuwa, masuala hayo yataliwezesha Baraza lako Tukufu kuishauri ipasavyo Serikali kuhusu namna bora ya kutunga na kuboresha baadhi ya Kanuni hizo, ili kuleta ufanisi wa utekelezaji wa Sheria husika.

**Mheshimiwa Spika,** kwa lengo la kuliwezesha Baraza lako Tukufu kuona maeneo ya kisheria yenye hoja mahsusi kwa ajili ya kushauri ipasavyo, Kamati ilichambua na Kujadili jumla ya kanuni 12 zilizowasilishwa kwenye Kamati hii na kubaini kuwa, jumla ya Kanuni 8 zilihitaji kufanyiwa maboresho ya kina na Kanuni tatu(4) zilihitaji kufutwa kabisa na kuandikwa upya kutokana na mantiki ya maudhui ya kanuni hizo kukosa uhalisia wa utekelezaji wake kwenye Jamii kwa mujibu wa sheria husika. Kanuni ambazo zilitakiwa kufutwa ni kama ifuatavyo:

**1.** Kanuni za Utumishi za Shirika ZBC, 2021

**2.** Kanuni za Utumishi za Benki ya Watu wa Zanzibar, 2022

3. Kanuni za Ushuru wa Huduma za Baraza la Manispaa Mjini, 2022

4. Kanuni za Usafi na Adhabu za Papo kwa Papo, 2021

**Mheshimiwa Spika,** kwa msingi huo wa uchambuzi, naomba kulitaarifu Baraza lako Tukufu kuwa,

hadi Kamati inakamilisha uchambuzi wa Kanuni hizi kwa mwaka 2022-2023, jumla ya masuala Mahsusi Matatu (3) yaliibua mjadala wa kipekee katika Kamati. Masuala hayo ni haya yafuatayo:-

**a) Ukiukwaji wa Sheria kwa ya maeneo katika Kanuni mbalimbali kama ifuatavyo;**

**Mheshimiwa Spika,** sheria zote zinazotungwa katika nchi ni lazima kufuata mtiririko wa kisheria na kutokwenda kinyume na sheria iliyojuu ya sheria husika. Kwa utaratibu huu endapo sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi itaenda kinyume na matakwa au maudhui ya Katiba ya Nchi basi sheria hiyo itakua imeenda kinyume na Mahakama itahitajika kuifuta sheria ile, utaratibu huohuo ndio unaotumika katika kanuni na sheria ndogo ndogo pale zitakapokwenda kinyume na sheria mama au sheria nyengine za nchi zilizotungwa na Baraza la Wawakilishi, kitendo hiko kitaalamu kinajulikana kama *ultra vires*. Neno hilo linatumika kuelezea kitendo kinachohitaji mamlaka ya kisheria au uwezo lakini kukafanyika nje ya mamlaka inayohitajika. Mheshimiwa Spika, kifungu cha 42 cha Sheria ya Tafasiri, 1984, imezuia Kanuni kwenda nje ya yaliyoainishwa na sheria mama, katika uchambuzi wa kanuni uliofanywa tumebainisha kanuni mbalimbali zilizokwenda nje ya mamlaka ya kisheria. Baadhi ya Kanuni hizo ni kama ifuatavyo;

**I.** Tafasiri ya neno *Baraza* ndani ya **Kanuni ya Usafi na Adhabu za Papo kwa Papo, 2021** ni tofauti na tafasiri iliyotolewa na **Sheria Nam 7 ya 2014** ambapo sheria imetafasiri neno Baraza kama Baraza lililoanzishwa kwa mujibu wa Sheria mama na Kanuni. Hata hiyo, Kanuni imetafasiri Baraza maana yake ni Baraza la madiwani ambalo limeanzishwa ndani ya Mamlaka ya serikali za Mitaa.

**II.** Mamlaka yaliyotolewa kwa Afisa Aliyeidhinishwa chini ya Kanuni ya 5(2) ya **Kanuni ya Usafi na Adhabu za Papo kwa Papo, 2021** ni zaidi ya mamlaka ambayo ameidhinishiwa Afisa huyo kwenye kifungu cha 63 cha **Sheria Nam 7 ya 2014.**

**III.** Jadweli la namba 15, 20 na 70 la ya **Kanuni ya Usafi na Adhabu za Papo kwa Papo, 2021**

linakwenda kinyume na matakwa ya **Sheria ya Wakala wa Barabara, Zanzibar Nam 11 ya 2019** na **Sheria ya Mipango Miji na Vijiji sura ya 85 ya mwaka 1955 na kanuni no 38/2015**

**IV.** Taratibu za upatikanaji wa ushahidi uliainishwa katika **kanuni ya 50 ya Kanuni za Mwenendo wa Mahakama ya Kadhi, 2021** unaenda kinyume na utaratibu wa kiislamu wa upatikanaji wa ushahidi ulioanishwa katika **kifungu cha 6 cha Sheria ya Mahakama ya Kadhi, Nam 9 ya 2017**

**V.** Taratibu za uajiri zilivyoainishwa katika **Kanuni ya 11(2) Kanuni za Utumishi za Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar, 2006** yenye kuielekeza Mamlaka kwa kushauriana na Bodi kuwasilisha kwa Kamisheni ya Utumishi wa Umma matokeo ya usaili wa wanaotaka kuajiriwa na mamlaka ni kwenda kinyume ya maelekezo ya **Kifungu cha 25 cha Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011**

**VI.** Mamlaka za uhamisho zilivyoainishwa katika **Kanuni ya 21(1) ya Kanuni za Utumishi za Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar, 2006** zinazompa mamlaka Mkurugenzi wa Idara kumuhamisha mfanyakazi kwa idhini ya Bodi ni kinyume cha taratibu za kimamlaka ya utumishi wa Umma kama zilivyoainishwa katika **Kifungu cha 10(1) cha Sheria ya Utumishi wa Umma, Nam. 2 ya 2011**

VII. Kanuni ya 119 ya **Kanuni za Utumishi za Shirika (ZBC), 2021** imeelezea kuhusu makosa yanayopelekea mtumishi kufukuzwa kazi. Hata hivyo jadweli la kwanza la **Sheria ya Utumishi wa Umma namba 2, 2011** linaelekeza mtumishi atakaetenda kosa hilohilo adhabu yake ni kuonywa na sio kufukuzwa kama ilivyoainishwa katika kanuni hiyo.

VIII. **Kanuni ya 90 ya Kanuni za Utumishi za Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, 2016** imeweka

ukomo wa siku saba (7) za kukata rufaa kwa mtumishi yoyote ambae hakuridhika na maamuzi dhidi yake kwa mujibu wa masharti ya Kanuni hizi. Hata hivyo, **Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Madai** ***(Cap 8 of the laws of Zanzibar) na*** **sheria ya Ukomo** ***(the limitation Act)*** zimeweka ukomo wa siku 30 za kukata rufaa tofauti na ukomo ulioainishwa katika kanuni hiyo.

**b. Matumizi ya lugha katika Kanuni mbalimbali zilizopitiwa.**

**Mheshimiwa Spika,** uandishi wa sheria ni nyezo muhimu katika mawasiliano ya kisheria. Mwandishi wa kisheria ni lazima kujua matumizi ya lugha na upangaji wa maneno kama ni nyezo muhimu sana katika utungaji wa sheria ili kutoleta utata katika utekelezwaji wa sheria hiyo. Hivyo, Mheshimiwa Spika, uandishi wa Kanuni kama ilivyo kwa sheria nyenginezo unahitaji mambo yafutayo;

1. **Uweledi wa maeneo ya sheria husika: Mheshimiwa Spika,** ni muhimu sana kwa mwandishi kuwa na uelewa wa kutosha katika eneo hilo ambalo anataka kuandikia sheria husika. Uweledi wa mwandishi katika sheria unapelekea kutumia lugha rafiki kufikisha ujumbe kwa walengwa kupitia maandiko ya sheria hiyo

2. **Matumizi ya lugha nyepesi: Mheshimiwa Spika,** nyezo muhimu inayotumika kupata kukifahamu kifungu cha sheria au kanuni ni kuangalia maana halisi ya maneno yaliyotumika katika kifungu hicho. Na pale ambapo itakosekana maana halisi ya maneno yaliyotumika katika kifungu hiko hulazimisha kutumika kwa tafasiri pana ili kutafuta maana iliyokusudiwa, hivyo Mahakama hutoa tafasiri ili kuondosha utata. Na wakati mwengine ugumu wa maneno hupelekea Mahakama kutoa miongozo tofauti na dhana ili iliyoandikwa katika kifungu husika.

**Mheshimiwa Spika,** makosa ya kiuandishi yaliyoibuliwa na Kamati wakati wa uchambuzi wa Kanuni zilizowasilishwa, baadhi yao yaliibua mvutano wa kimaana ndani ya kamati ili tu kupata maana halisi

ya kanuni husika. Baadhi ya maneno hayo ni kama yafuatayo:

i. Maneno **'Mdaawa na Wadaawa'** yaliyotumika sana katika **Kanuni za Mwenendo wa Mahakama ya Kadhi, 2022** yalikosa tafasiri na kupelekea kamati kuwa na uelewa tofauti na dhana iliyokusudiwa katika kanuni ambazo maneno hayo yalitumika

**ii.** Maneno **'Kujazaa barua'** yanayoonekana sehemu mbalimbali kwenye **Kanuni za Utumishi za Shirika la Bandari Zanzibar, 2012** yalimaanisha kujaza fomu

**iii.** Maneno mbalimbali yaliyotumika katika **Kanuni za Utumishi za Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar, 2006** yametolewa tafasiri tofauti katika sheria husika, mfano, *Rushwa, Udanganyifu, Madawa ya Kulevya* na Kadhalika

c. **Makosa ya kisarufi**

**Mheshimiwa Spika,** kama ambavyo Kamati imeeleza katika ripoti yake iliyopita, ni jukumu la ofisi ya Mwanasheria Mkuu kuipitia Kanuni ile na kuondosha yale makosa ya kisarufi (typos) na makosa mengine ya kimantiki kwa kuwa mara baada ya Wakala wa Uchapaji kuchapisha nakala za awali huwasilisha Ofisi ya Mwnasheria Mkuu na si kwa mteja na baada ya kupata ithibati Wakala huchapisha kanuni zilizohaririwa. Hata hivyo, bila ya Kamati kupata jibu sahihi wakati wa uchambuzi wa kanuni mbalimbali, kanuni nyingi zimeendelea kuwa na makosa ya kiherufi kama ilivyoainishwa katika majadueli yaliyoambatanishwa na ripoti hii.

## Sehemu ya Nne

## Ziara za Kamati

**Mheshimiwa Spika,** katika mzunguko huu wa 2022/23 Kamati iliweza kufanya ziara tatu (3) Tanzania Bara zenye maudhui tofauti. Katika ziara hizo kamati ilipata fursa ya kutembelea taasisi zifuatazo:

1. Shirika la Utangazaji Zanzibar, Dar es Salam
2. Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Tanzania (NSSF)
3. Mamlaka ya Bandari, Dar es Salam
4. Mamlaka ya Viwanja Vya Ndege, Dar es Salam
5. Kampuni ya Uendeshaji wa Uwanja wa Ndege wa Kilimanjaro (KADCO)

**Mheshimiwa Spika,** baadhi ya ziara hizi zilitokana na kazi ya upitiaji wa kanuni za Utumishi zinazohusiana na Taasisi zilizoainishwa hapo juu ili kuona wenzetu wanatatuaje changamoto zao kitumishi katika utekelezaji wa kanuni zao.

**1. Shirika la Utangazaji Zanzibar, Dar es Salam**

**Mheshimiwa Spika,** katika kupitia **Kanuni za Utumishi za Shirika ZBC, 2021** Kamati ilihitaji kupata mawazo ya wadau wanaohusika na Kanuni hiyo ili kujua changamoto mbalimbali wanazokutana nazo katika utekelezwaji wa matakwa ya kanuni hiyo. Hivyo, Kamati iliweza kukutana na watendaji wa Shirika la Utangazaji ZBC kwa upande wa Zanzibar, Pemba na Dar es Salam.

**Mheshimiwa Spika,** katika ziara hiyo, Kamati iliweza kugundua mambo yafuatayo:

i. Wafanyakazi walipo Dar es Salam kutokujua uwepo wa Kanuni za Utumishi zinazowaongoza wao katika utendaji na maslahi yao ndani ya Shirika,

ii. Wafanyakazi hazo kwa muda mrefu wameshindwa kupata maslahi yao kwa mujibu wa

masharti ya Kanuni hizi,

iii. Kutokuwepo kwa ushirikishwaji wa kiuongozi ndani ya Kanuni baina ya Shirika kwa upande wa Zanzibar na Tanzania Bara. Mtiririko wa Kiuongozi na hata katika vikao vya utendaji wa Shirika haumjumuishi Mkuu wa Shirika hilo Dar es Salam.

iv. Mapungufu ya kikanuni kuzorotesha utendaji wa Shirika hususan kwa upande wa Tanzania Bara ambapo ushindani wa vyombo vya Habari ni mkubwa zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni za Utumishi za Taasisi mbalimbali zimetungwa kwa kuzingatia masharti ya **Sheria ya Utumishi ya mwaka 2012** pamoja na **Kanuni za Utumishi za mwaka 2014** ili kuweka taratibu sahihi za kiutumishi kulingana na mazingira ya taasisi husika. Shirika la Utangazaji la ZBC ni miongoni mwa taasisi ambazo kupitia Bodi ya Shirika ilitunga Kanuni hizo kwa lengo la kuweka njia sahihi ya kiutumishi pamoja na kutatua changamoto mbalimbali za watumishi wa Shirika.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilisikitika sana kuona kuwa watendaji walio wengi hawakuwahi kuijua kanuni hiyo na wala hawakuweza kutoa maoni yao katika uandishi wa Kanuni hiyo iliyotungwa mwaka 2021. Mhe. Spika, utaratibu wa kutunga sheria haukubali kwa mtu mmoja au kikundi cha watu wachache kujifungia ndani na kuweka masharti yanayogusa maslahi ya watu pamoja na kuweka taratibu za kinidhamu bila ya kuchukua maoni ya wadau ambao ndio wanufaikaji wa masharti hayo.

**Mheshimiwa Spika,** kamati, Uongozi wa Wizara pamoja na Bodi ya Shirika katika ziara hiyo ilisikitishwa sana na hali ya kiutendaji wa shirika hilo, aidha, kwa pamoja tuliweza kuona mapungufu makubwa ya Sheria ya ZBC pamoja na kanuni ya Shirika kuwa zimeshindwa kutatua changamoto zinazowakabili watendaji wa shirika hilo.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na mgongano uliopo katika ya sheria na kanuni hii kama ilivyoelezwa katika sehemu zilizopita, pamoja na kasoro hizo zilizoainshwa awali, Kamati kwa mashauriano mazuri

na Wizara pamoja na Bodi ya Shirika tulikubaliana kuifuta kanuni hiyo na kuitaka Bodi kuanza mchakato bora wa kutunga kanuni zitakazolipa uhai na uweledi shirika hilo kuweza kukabiliana na ushindani uliopo. Aidha, Kamati pia iliielekeza Wizara kuangalia uwezekano wa kuifanyia marekebisho sheria inayoanzisha Shirika la Utangazaji Zanzibar ili kuendana na mazingira yaliyopo sasa.

**2. Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Tanzania (NSSF)**

**Mheshimiwa Spika,** tunafahamu ya kuwa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii umebeba dhima ya kuwahudumia wafanyakazi baada ya kustaafu kupitia michango yao wanayoweka kila mwezi kupitia waajiri wao. Kamati iliweza kupitia **Kanuni za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar, 2007 (pamoja na marekebisho ya 2017)** ambapo changamoto kadhaa za kiutendaji zilijitokeza katika majadiliano, baadhi ya changamoto hizo ni kama zifuatazo:

i. Taratibu za uwekezaji kupia ZSSF
ii. Taratibu za malipo ya Mafao
iii. Muelekeo wa Mfuko kwa miaka 50 ijayo
iv. Muundo wa Mfuko
v. Haja ya kuwa na Mfuko wa fidia kwa mfanyakazi

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata fursa ya kutembelea mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii **(NSSF)** pamoja na Mfuko wa Fidia kwa wafanyakazi **(WCF)**. Katika ziara hiyo, Kamati na Uongozi wa ZSSF tuliweza kujifunza mengi kuhusu uendeshaji wa mifuko miwili hiyo pamoja taratibu zao za uwekezaji. Kamati imegundua kuwa ZSSF kwa upande wa Mfuko wa Hifadhi inaonekana kutenda vyema hasa kupitia ripoti ya mtathmini iliyotolewa *(Actuarial Report).*

**Mheshimiwa Spika,** jambo kubwa ambalo tumejifunza kwa kupande wa Tanzania Bara ni uendeshaji

tofauti wa Mifuko hiyo miwili ambayo imeanzishwa kwa sheria mbili tofauti na kuwa na kanuni mbili tofauti zinazoratibu Mifuko hiyo. Moja ya tofauti ya Mifuko hiyo ni kuwa NSSF ni kwa wafanyakazi wa Umma tu ila WCF inabeba wafanyakazi wote pamoja na wale wa binafsi.

**Mheshimiwa Spika,** matunda ya ziara hiyo ni kuletwa kwa mabadiliko ya **Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Nam 2 ya 2005** ambayo yamelenga kuanzisha mfuko wa fidia kwa wafanyakazi wa umma na binafsi kwa upande wa Zanzibar, hadi hapa tunapowasilisha ripoti hii ZSSF imefanikiwa kutunga **Kanuni za Fao la Upotevu wa Ajira, 2022** na pia imeshakamilisha mchakato wa kutunga Kanuni ya **Kanuni za Fao la Kuumia Kazini,2023** ambazo zote kwa pamoja zinategemewa kuwasilishwa mbele ya Kamati kwa lengo la kupitiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaupongeza sana Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kupitia Mkurugenzi Mtendaji Bwana Nassor Shaaban Ameir na timu yake ya Uongozi kwa mafanikio makubwa yaliyopatikana ndani ya muda mfupi. Tunaamini utungwaji wa Kanuni hizo kutasaidia kuboresha maisha ya wafanyakazi katika visiwa vyetu haswa pale wanapopoteza ajira zao.

**3. Mamlaka ya Bandari, Dar es Salam**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati hii ilipata fursa ya kukutana na watendaji mbalimbali wa Shirika la Bandari la Zanzibar wakati wa kupitia **Kanuni za Utumishi za Shirika la Bandari Zanzibar, 2012**. Watendaji hao ambao ndio wadau wa Kanuni hii waliainisha changamoto mbalimbali zilizomo katika Kanuni na zile ambazo zinatokea nje ya matakwa ya Kanuni. Baadhi ya changamoto hizo ni kama ifuatavyo;

i. Chama cha Wafanyakazi wa bandari kutopata fursa ya kushiriki katika maamuzi yanayohusu utendaji wa Shirika

ii. Maslahi ya watendaji kutopatikana ipaswavyo kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma,

2012

iii. Uwepo wa mgogoro kati ya uongozi wa shirika na wafanyakazi wa kada za usafi na ulinzi ambao wanafanyakazi kwa malipo ya kila siku

iv. Kutokufahamika kisheria muingiliano kati ya Shirika la Bandari na Kampuni ya inayofanya kazi za usafi inayojulikana kama Jitihada njema.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na changamoto mbalimbali zilizoibuliwa katika upitiaji wa kanuni hiyo, Kamati kwa kushauriana na Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi pamoja na uongozi wa Shirika la Bandari tulikubaliana tuangalie wenzetu Mamlaka ya Bandari Tanzania wamewezaje kutatua changamoto za watendaji wao na kuongeza ufanisi wa mamlaka hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** kamati hii iliweza kukutana na uongozi wa Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) pamoja na kupata fursa ya kuangalia shughuli mbalimbali zinazofanywa na watendaji wa mamlaka hayo wakiwemo wafanyakazi wa malipo ya kila siku (*daily paid)*. Miongoni mwa mambo ambayo Kamati imejifunza ni kama yafuatayo:

**i.** Bodi ya Mamlaka ya Bandari ipo kiushauri na si kiutendaji *(Advisory Board)*. Uwepo wa Bodi yenye mamlaka ya kiutendaji *(Executive Board)* kunazorotesha na kuongeza urasimu wa majukumu ya bandari ambayo ipo kibiashara na ushindani katika kutoa huduma zake kwenye ukanda wa pwani ya mashariki. Mheshimiwa Spika, Bodi ya Shirika la Bandari la Zanzibar ilimaliza muda wake tangu mwaka 2022 hivyo, kwa taratibu za kiutendaji maamuzi ya shirika hilo yanakwenda kwa Katibu Mkuu wa Wizara hadi pale Bodi itakapoteuliwa na kutekeleza majukumu yake kisheria.

**ii.** Kutokuwepo maingiliano ya kiutendaji kati ya Mamlaka ya Bandari na Bodi ya Bandari.

**iii.** Mkurugenzi wa bandari ya Dar es Salam na Mameneja wa Bandari mbalimbali husimamia

utendaji wa Bandari zao bila ya kuingiliwa na Mamlaka ya Bandari. Hata hivyo hutakiwa kuwasilisha ripoti za utendaji wao kwa Mkurugenzi Mkuu

**iv.** Utenguzi wa mamlaka na utendaji wa Mkurugezi Mkuu na Naibu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Bandari

**v.** Uwepo wa mamlaka ya kuajiri wafanyakazi wa vibarua *(daily paid)* kutoka kampuni tofauti kulingana na mahitaji ya Mamlaka hiyo

**vi.** Kuongeza maslahi ya watumishi ikiwemo bima kubwa ya afya pamoja na posho mbalimbali kuhamasisha watendaji kufanyakazi kwa weledi kwa saa 24

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na tuliyojifunza kwa wenzetu wa Mamlaka ya Bandari Tanzania, pamoja na changamoto zilizoibuliwa na watendaji wa Shirika la Bandari Zanzibar ni dhahiri kuwa kuna haja ya kuifanyia mapitio sheria yetu ya bandari na kanuni zake ili kuweza kuakisi matakwa ya wakati tulionao pamoja na ushindani uliopo. Hivyo Kamati ililielekeza Shirika la Bandari kuanza mchakato wa kufanyia marekebisho sheria pamoja na kutunga kanuni mpya itakayoliwezesha Shirika kukuwa kiutendaji na hatimae Zanzibar kurudi kwenye ushindani wa kibiashara kupitia Bandari yetu.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kulifahamisha Baraza lako tukufu kupitia ripoti hii kuwa agizo lililotolewa na kamati tayari limeshaanza kufanyiwa kazi ambapo kwa taarifa tuliyopokea tayari hatua za awali za mchakato wa marekebisho ya Sheria na Kanuni za Bandari zimeanza kutekelezwa. Hivyo, kwa dhati kabisa tunampongeza Mkurugenzi Mkuu wa Shirika, Naibu Mkurugenzi Mkuu na timu yao kwa kutekeleza yale yalioamriwa na Kamati kwa manufaa ya umma.

**4. Mamlaka ya Viwanja Vya Ndege Tanzania**

**Mheshimiwa Spika,** tulipokuwa tuapitia **Kanuni za Utumishi za Mamlaka ya Viwanja vya ndege Zanzibar, 2016** mambo mbalimbali yalizua mjadala ndani ya Kamati na hata wakati wa majadiliano na Wadau ambao ni watumishi wa Mamlaka. Miongoni mwa yaliyoibua mjadala ni kama yafuatayo:

**i. Utaratibu wa utumishi wa mikataba**

**i. Migogoro ya Mikataba ya Utumishi**

**Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar kwa muda mrefu ilikua na mgogoro unaohusisha taratibu za utumishi kwa wafanyakazi wa mikataba. Utaratibu huu ambao umejumuisha kundi la wafanyakazi wengi katika maeneo mbalimbali ya viwanja vya ndege kwa upande wa Unguja na Pemba. Kanuni za utumishi za Mamlaka hazijawatambua wafanyakazi hao wa mikataba pamoja na stahiki zao kama ambavyo walivyotambuliwa katika kifungu cha 60(1)(c) cha Sheria ya Utumishi wa Umma, 2012.

**ii. Haki na fursa za wafanyakazi**

**Mheshimiwa Spika, Kanuni za Utumishi za Mamlaka ya Viwanja vya ndege Zanzibar, 2016** zimeainisha haki na fursa nyingi ambazo wafanyakazi wa Mamlaka wanatakiwa kuzipata ikiwemo posho mbalimbali kama *night allowance,* posho la kazi za mazingira magumu, posho za muda wa ziada na mengineyo. Hata hivyo malalamiko mengi ya wafanyakazi yanahusisha kutokulipwa kwa stahiki hizo. Aidha wafanyakazi wamekosa fursa za mafunzo pamoja na stahiki nyenginezo.

**Mheshimiwa Spika,** majadiliano mapana kati ya Kamati, uongozi wa Wizara pamoja na Mamlaka ya Viwanja vya ndege Zanzibar tuliweza kutatua baadhi ya changamoto hizo kama ifuatavyo;

**i.** Wafanyakazi wa mikataba kupata fursa sawa na wafanyakazi wengine ikiwemo malipo ya likizo ya kawaida na ili ya uzazi, posho mbalimbali na kadhalika

**ii.** Wafanyakazi wanaofanyakazi katika mazingira hatarishi kama mionzi na waongoza ndege wamewekewa utaratibu maalumu wa stahiki zao

**iii.** Muda wa ziada kulipwa kwa utaratibu maalumu.

**Mheshimiwa Spika,** tulipofanya ziara ya kutembelea Mamlaka ya Viwanja vya ndege Tanzania tuligundua kuwa Mamlaka ya Viwanja vya ndege Zanzibar imepiga hatua sana kiutumishi kuliko Mamlaka ya Tanzania**(TAA)**. TAA inasimama kama wakala wa Serikali katika kuendesha viwanja vya ndege Tanzania, katika muktadha huo, TAA haina mamlaka kuajiri mfanyakazi yoyote wala kupanga maslahi ya mfanyakazi yoyote. Tofauti na ZAA, Katibu mkuu wizara ya Uchukuzi ndie Afisa Masuli ***Accounting Officer*** wa TAA.

**5. Kampuni ya Uendeshaji wa Uwanja wa Ndege wa Kilimanjaro (KADCO)**

**Mheshimiwa Spika,** uwanja wa ndege wa Kilimanjaro unaendeshwa na Kampuni ya **KADCO** ambayo inamilikiwa kwa asilimia 100% na Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. Uwanja huu haupo chini ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA), bali unaendeshwa katika mfumo wa Kikampuni ambapo Mkurugenzi Mtendaji ndie mwenye maamuzi ya kiutendaji chini ya usimamizi wa Bodi ya Ushauri.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pamoja na viongozi wa ZAA imejifunza mengi katika ziara hii yatakayowezesha Mamlaka kupanua wigo wa utendaji katika viwanja vya ndege Zanzibar. Miongoni mwa yaliyojitokeza ni kama yafutayo:

**i. Kurahisishwa utekelezwaji wa matakwa mbalimbali:**

**Mheshimiwa Spika,** moja ya mafanikio makubwa yaliyopatikana katika uwanja wa ndege wa Kilimanjaro ni uondoshwaji wa urasimu katika mambo mbalimbali yanayohusu maendeleo ya uwanja. Mambo yote yanayoamuliwa kutekelezwa yanaamuliwa na Mkurugenzi Mtendaji kwa ridhaa ya Bodi bila ya kupita Wizarani. Utaratibu huu hurahishisha utekelezaji wa mambo yanapangwa kutekelezwa kwa wakati unaohitajika.

### ii. Uboreshwaji wa Maslahi ya Watumishi

**Mheshimiwa Spika,** KADCO yenyewe ndio inayopanga bajeti yake na kuiwasilishwa Wizarani kwa lengo la kuchanganywa na Bajeti kuu. Hivyo, KADCO imekuwa ikiangalia maboresho ya maslahi na motisha kwa wafanyakazi waka mara kwa mara ili kuboresha ari ya kiutedaji.

### iii. Umiliki wa Mapato yanayotokana na uendeshaji wa Uwanja

**Mheshimiwa Spika,** Serikali kupitia Msajili wa Hazina hupokea gawio linalotokana na faida iliyopatikana katika mapato yaliyokusanywa. KADCO imefungua akaunti zake Benki Kuu ya Tanzania (BOT) ambapo mapato na matumizi hufanyika kupitia akaunti hizo.

**Mheshimiwa Spika,** mafanikio yaliyopatikana KIA yameufanya uwanja huo kuwa ni wa pili kwa uwendeshaji Tanzania baada ya Uwanja wa Kimataifa wa Julius Nyerere. Hivyo, Kamati imeitaka ZAA kuangalia maeneo ya Sheria na Kanuni za Mamlaka ambayo kwa mazingira yetu yataruhusu kurekebishwa ili kuzidisha ufanisi na kuboresha huduma za Mamlaka.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatoa pongezi za dhati kabisa kwa Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar, Ndugu Seif Juma pamoja na timu yake ya uongozi kwa jitihada wanazochukua kutatua changamoto za wafanyakazi zilizodumu kwa muda mrefu. Hakika kiongozi wa aina hii ndie anaehitajika katika taasisi zetu ili kuleta chachu ya maendeleo inayoendana na dira na muelekeo wa Mhe. Rais wa Zanzibar, Dr. Hussein Ali Mwinyi na ilani ya Chama cha Mapinduzi.

## Sehemu ya Tano

## Mapendekezo ya Kamati

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaendelea kushauri mamlaka zote ambazo zimekasimiwa na Baraza la Wawakilishi madaraka ya kutunga Kanuni na Sheria Ndogo ndogo, kuzingatia kikamilifu ushirikishwaji wa wadau wanaolengwa na Kanuni na Sheria Ndogo ndogo yoyote ili kupunguza changamoto mbalimbali zinazoweza kujitokeza wakati wa utekelezaji wa Kanuni au Sheria Ndogo hizo.

**Mheshimiwa Spika,** kamati inashauri Serikali kupitia Afisi ya Mwanasheria Mkuu iongeza idadi ya Mawakili wa Serikali katika Ofisi Taasisi mbalimbali na hasa vitengo vinavyohusika na upitiaji wa Kanuni na Sheria Ndogo ndogo ili kuhakikisha kuwa Taasisi hizo zinatumia mamlaka yake kisheria ya kutunga Kanuni na Sheria ndogo kwa mujibu wa Sheria. Aidha Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa stahiki za Mawakili na Wanasheria wa Serikali wanapata stahiki zao na kuwekewa mazingira mazuri ya utendaji ili kurahisisha majukumu yao ambayo kimsingi ndio yanayoendesha nchi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Mamlaka zilizopewa jukumu la kutunga Kanuni na Sheria Ndogo ndogo kufanya kazi kwa karibu na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wakati wa utungaji wa Kanuni na Sheria Ndogo ndogo kwa lengo la kuondoa dosari mbalimbali zinazojitokeza.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuchukua hatua za haraka kuzifanyia marekebisho Kanuni na Sheria Ndogo ndogo zote zenye dosari. Baada ya marekebisho hayo kufanyika na kuchapishwa katika Gazeti la Serikali, Kanuni na Sheria Ndogo ndogo hizo ziwasilishwe Baraza la Wawakilishi kwa mujibu wa Sheria.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imegundua kuwa baadhi ya Taasisi hususan zile ambazo zimekasimiwa mamlaka ya kutunga sheria ndogo kutumia vibaya mamlaka hayo kwa kutunga sheria ndogo zinazoenda kinyume na mamlaka yao yaliyoainshwa katika sheria. Kuendelea kufanya hivyo ni kukiuka msingi

mkuu wa ugawaji wa mamlaka na kuingilia utendaji wa Taasisi nyengine ambapo mwananchi ndie anakua muathirika. Mfano wa hili ni pale mamlaka ya serikali za mitaa kutaka kupora mamlaka ya Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) katika ukusanyaji wa ushuru wa asilimia 3 kwa bidhaa zinazozalishwa au huduma zinazotolewa.

**Mheshimiwa Spika**, licha ya kuwa Kamati kwa kiasi kikubwa imejiridhisha kwamba Kanuni zimefuata taratibu za utungaji ingawaje kumejitokeza kwa baadhi ya Kanuni kukosekana ushirikishwaji wa Wadau walio wengi wakati wa utungaji wake jambo ambalo ni kasoro kubwa kwa Kanuni hizo hasa ukizingatia kwamba zinagusa maisha ya kila siku ya kila mmoja wetu. Hivyo tunazitaka taasisi zote kushirikisha wadau ipasavyo katika utungaji wa Kanuni na Sheria ndogondogo

## HOJA ZA KAMATI

### a. Kupitwa na wakati kwa sheria mbalimbali Zanzibar

Kwamba, sheria mbalimbali zimeshapitwa na wakati na kufanya kushindwa kufanyakazi kikamilifu kwa nyakati za sasa na kupelekea kanuni mbalimbali kushindwa kuwa na nguvu katika kuleta maendeleo nchini

### b. Kukinzana na masharti ya Sheria Mama au Sheria nyingine za nchi.

Kwamba, baadhi ya Kanuni na Sheria Ndogo ndogo zilizofanyiwa uchambuzi na Kamati zilibainika kuwa na vifungu vinavyokinzana na masharti ya Sheria Mama na Sherianyingine za nchi.

### c. Dosari ya Uandishi wa Majedwali ikilinganishwa na Vifungu vya Sheria

Kwamba, katika uchambuzi wa Kamati imebainika kuwa baadhi ya Kanuni na Sheria Ndogo ndogo zina dosari mbalimbali.Na Kwamba, kukinzana huko kunaifanya Kanuni husika kuwa ni batili kwa kiwango

ilichokinzana.

Hivyo Basi, Baraza la Wawakilishi linaazimia kwamba, Wizara zinazohusika, kufanya marekebisho katika Kanuni na Sheria Ndogo ndogo hizo ili kuondoa vifungu vinavyokwenda kinyume na masharti ya Sheria Mama na Sheria nyingine za nchi.

## Sehemu ya Sita

## HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na Baraza lako tukufu kwa kuendelea kutuamini na kutupa nafasi sisi wajumbe wako kuendelea kuhudumu katika Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo ndogo na kutuwezesha leo kuwasilishwa ripoti yetu katika Baraza lako tukufu. Ni matumaini yetu kuwa, utaratibu huu utakuwa endelevu na umuhimu wa Kamati hii na Kamati nyenginezo katika maendeleo ya nchi yetu. Aidha tunaishukuru Afisi ya Katibu wa Baraza na wasaidizi wake kwa kuhakikisha kuwa uwepo wa Kamati ya Kanuni na Sheria ndogo ndogo ni muhimu sana kwa kuwa kwa kiasi kikubwa Kanuni na Sheria Ndogo ndogo ndizo zinagusa maisha ya kila siku ya wananchi wengi.

**Mheshimiwa Spika,** kipekee kabisa naomba nimshukuru Mhe. Haroun Ali Suleiman, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na Mhe. Dr. Mwinyi Haji Talib (Mwanasheria Mkuu) wote kwa pamoja walishirikiana nasi kupitia maafisa wao kufanikisha majukumu yetu kwa urahisi. Aidha, niwashukuru Mawaziri, Makatibu Wakuu na Wakuu wa Sekta mbalimbali kwa kufika mbele ya Kamati na kujibu hoja zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati. Aidha , naomba nimshukuru Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar, Mkurugenzi wa Shirika la Bandari la Zanzibar na Mkurugenzi wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar wote hawa kwa mashirikiano waliyoipa Kamati kufanikisha kazi ambayo italeta tija kwa maendeleo ya Zanzibar na watu wake.

**Mheshimiwa Spika,** kabla sijahitimisha naomba kuitanabahisha Serikali kuwa Kamati hii haina tatizo wala mkwaruzani na Serikali kama ambavyo baadhi ya Maofisa wanavyochukulia tofauti pale ambapo tunapotumia mamlaka yetu ya kikanuni yaliyozaliwa na Katiba ya Zanzibar kuhoji na kushauri katika

kanuni ambazo zinawasilishwa kwetu.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa heshima na taadhima sasa naomba niwatambue kwa jinsi walivyofika mbele ya Kamati kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Masoud Ali Mohammed (MBM) – Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ
2. Mhe. Tabia Maulid Mwita (MBM) – Waziri wa Habari,Vijana, Utamaduni na Michezo Zanzibar
3. Mh. Haroun Ali Suleiman, (MBM)-Waziri wa Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Zanzibar
4. Mhe. Dr. Khalid Salum (MBM) - Waziri wa Ujenzi, mawasiano na Uchukuzi

**Mheshimiwa Spika**, kwa kipekee kabisa nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo ndogo kwa kazi kubwa na nzuri ya kuchambua Kanuni na Sheria Ndogo ndogo zilizowasilishwa mwaka 2022 na hatimaye kufanikisha kazi hii. Wajumbe wa Kamatihii ni kama ifuatavyo;

1. Mhe. Mihayo Juma N'hunga – Mwenyekiti
2. Mhe. Zawadi Amour Nassor - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma - Mjumbe
4. Mhe. Kombo Mwinyi Shehe - Mjumbe
5. Mhe. Mohammed Ahmada Salum - Mjumbe
6. Mhe, Hudhaima Mbarak Tahir - Mjumbe
7. Mhe. Issa Haji Gavu - Mjumbe
8. Ndg. Karima Abdulwahab - Katibu
9. Ndg. Abdu Maulid Haji - Katibu

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

**Mhe. Mihayo Juma N'hunga,**

**Mwenyekiti**

**Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo**

**Baraza la Wawakilishi**

**Febuari, 2023**

# VIAMBATANISHO

**Kiambatanisho No. 1**

**MAREKEBISHO YA JUMLA YA KANUNI ZA SHIRIKA LA BANDARI LA ZANZIBAR**

Kamati baada ya kupitia Kanuni hii kwa kina pamoja na kukutana na watendaji wa Shirika la bandari, ilibaini kasoro katika kanuni na changamoto mbali mbali zinazowakabili watendaji wa Shirika miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na:

- ✓ Kukosekana kwa uelewa kwa baadhi ya watendaji wa Shirika juu ya uwepo wa Kanuni ya Utumishi ya Shirika la Bandari.
- ✓ Kuwepo kwa wafanyakazi wa muda mrefu ambao uajira wao ni malipo ya siku (group C) ambao mpaka sasa hawaijui hatima yao.
- ✓ Kuwepo kwa wafanyakazi wachache wanaotoa huduma bila ya kulipwa fedha za kazi za saa ya ziada.
- ✓ Aidha, suala la bonus kwa watendaji nalo lilichukua nafasi katika malalamiko ya watendaji.

Mbali na hayo Kamati ilipata fursa ya kupitia Kanuni hiyo na kubaini mambo yafuatayo:

Kamati inahitaji ufafanuzi wa Kanuni ya 4, kuhusu **Katibu wa Mkurugenzi Mkuu** kuwa **Katibu wa Kamati Tendaji.**

Kuhusu Kanuni ya 5, Kamati inahitaji ufafanuzi kwani baadhi ya Majukumu ya bodi yanatekelezwa na Kamati Tendaji.

Kanuni ya 7, Kamati inataka kufahamu kwa nini Kamati ya Uongozi imepewa jukumu la **kusimamia nidhamu kama jukumu la msingi wakati suala la nidhamu ni sehemu tu ya majukumu yake**.

Pia, Kamati ya Uongozi inaonekana kuwa na wajumbe wengi kamati inashauri kupunguza wajumbe hao ili kupatikane ufanisi zaidi.

Aidha, suala ya Kamati hiyo kukutana mara moja kwa mwaka Kamati ya Kanuni inahitaji kufahamu ni upi msingi wa kukutana mara moja kwa mwaka.

Kuhusu suala ya **Mhasibu Mkuu** kuwa **Katibu wa Kamati** hiyo ni kinyume na utaratibu hivyo kamati

lirekebishwe.

**Kanuni ya 11** ambayo inazungumzia **masharti ya ajira** ihamishwe na kuwekwa badala yake katika **kanuni ya 13(4)** ambayo inazungumzia **kazi za Kamati Ajira** ambapo itasomeka kama ni aya ya (a) ya Kanuni hiyo kama ifuatavyo "**kuandaa masharti ya ajira kulingana na nafasi husika**". Aidha Kanuni ya (a) itasomeka (b) na zilizobaki zitafuata mpangilio wake.

1. Kanuni 13(b), Kamati inataka kufahamu ni nini madhumuni ya kuweingiza **wakurugezi wote** wa Shirika katika **Kamati ya Ajira** kwani inaweza kukosa **ufanisi mzuri wa kamati hiyo**.

Kanuni ya 61(2) Kamati inataka ipatiwe ufafanuzi kuhusu michango ya mfanyakazi aliyechangia katika mfuko wa hifadhi ya jamii utaratibu wake unakuwaje **(kwani fedha wanazozichangia ni za kwake hivyo utaratibu lazima uzingatie haki hiyo ya mfanyakazi)**

Kamati imebaini kwamba kanuni ya 84(2)(a) ipo kinyume na utaratibu wa **kanuni ya 61 ya Utumishi wa Umma** kwani likizo ya uzazi hutolewa baada ya mtumishi kujifungua.

Aidha,Kanuni ya 84(2)(b) nayo pia ina changamoto kwani suala la mapendekezo ya daktari ni suala linalochukuliwa kuwa ni ugonjwa na sio maombi yanayotokana na utashi au hiyari ya mfanyakazi kwa hivyo mfanyakazi asinyimwe haki yake ya likizo iwapo mapumziko yalipendekezwa na daktari.

Kanuni ya 16(5) ifanyiwe tafsiri ZPC1, ZPC2, ZPC3, ZPC4 na ZPC6. kwani fomu zote hizo zimeainishwa katika Jaweli la Pili la Kanuni hizi.

Kamati inashauri kwamba katika uandishi mzuri wa kisheria katika kuhakikisha kwamba kila panapozungumzia **aliyetenda kosa** kuwa **atawajibika** litangulie neno "**atakapopatikana na hatia"**.

## MAPENDEKEZO MAHSUSI YA MAREKEBISHO YA KANUNI ZA UTUMISHI YA SHIRIKA LA BANDARI LA ZANZIBAR

1. Katika kichwa cha habari cha sehemu ya kwanza neno **"UTANGULIZI**" linarekebishwa kwa kufuta na kuandika upya **"MASHARTI YA AWALI".**

2. Katika Kanuni ya 1, inarekebishwa kwa kufuta neno **“zitakapoidhinishwa”** na kuweka badala yake maneno **“kuweka saini”.**

3. Katika Kanuni ya 2, inarekebishwa kwa kufuta maneno “**ila pale**” na kuweka badala yake maneno **“isipokuwa pale”.**

4. Kanuni ya 3, inarekebishwa katika baadhi ya tafsini ya maneno:

5. **“hujuma ya kazi”** kwa kuingiza maneno **“au kwa uzembe**” baina ya neno **“makusudi”** na **“cha”.**

6. Kanuni ya 4(3) inarekebishwa kwa kufuta na kuandikwa upya kama ifuatavyo:

“**kamati itateua Afisa mwenye uzoefu usiopungua miaka mitatu kuwa katibu wa kamati**”.

7. Kanuni ya 7(1) inarekebishwa katika neno **“nidhamu”** na kuweka badala yake maneno **“mwenendo wa utumishi”** baina ya neno **“kusimamia”** na **“ndani”.**

8. Kanuni ya 7(4) inarekebishwa kwa kufuta “(f)” na kuweka badala yake “(e)”.

9. Kanuni ya 8(e) inarekebishwa kwa kufutwa maneno **“yanaboreshwa mara kwa mara”** na kuweka badala yake maneno “**yanaimarishwa kadiri hali inavyoruhusu”**

10. Kanuni ya 9 inarekebishwa kwa kufuta maneno “**kwa mwaka**” na kuweka badala yake maneno “**kila baada ya miezi mitatu”.**

11. Kanuni ya 12(3) inarekebishwa kwa kuifuta na kuandika upya kama ifuatavyo:

**“Shirika linaweza kumfanyia usaili mfanyakazi ili kuhakikisha uwezo wake kabla ya kuhamishwa kujaza nafasi iliyo wazi”.**

12. kanuni ya 13(1) inarekebishwa kwa kufuta maneno **“kufanya usaili wa waombaji wa”** na kuweka badala yake maneno **“kusimamia masuala yote ya”** baina ya neno **“la”** na **“ajira”.**

13. Kanuni ya 13 (3) inarekebishwa kwa kufuta maneno “**katika utekelezaji bora wa kazi zake”** yaliopo mwanzoni mwa Kanuni ndogo hiyo.

14. Kanuni 13(4) inarekebishwa kwa kuongeza aya ya (a) na (b) na kusomeka kama ifuatavyo:

a) **"kuandaa masharti ya ajira kulingana na aina ya ajira husika.**

b) **Bila kuathiri kanuni 13(4)(a) yafuatayo yatakuwa ni miongoni wa masharti ya ajira.**

i. **awe Mtanzania,**

ii. **awe na tabia nzuri na uwezo wa kufanya kazi,**

iii. **awe na afya iliyothibitishwa na daktari,**

iv. **aliyekuwa hakuwahi kutiwa hatiani kwa kosa la kutokuwa muaminifu au muadilifi**

v. **aliyekuwa hajawahi kufukuzwa kazi kwa kosa la utovu wa nidhamu na**

vi. **awe na sifa zilizowekwa katika ajira"**

Aidha, aya ya (a) ya awali kuwa (c) na ngenyine zitafuata mpangilio mpya wa aya hizo.

15. Kanuni ya 15 inarekebishwa kwa kufutwa. Aidha, Kamati inashauri kuwekwa katika Kanuni ya 13(a) mpya kama ni miongoni mwa masharti ya ajira. (**Kwani Sheria pamoja na Kanuni huandikwa kwa yale yanayohitajika).**

16. Kanuni ya 18(1) inarekebishwa kwa kufuta maneno **"kujazaa barua"** na kuweka badala yake "**kujaza fomu".** Aidha, marekebisho hayo yafanyike kila yanapojirejea maneno hayo ndani ya Kanuni hizi.

17. Kanuni ya 18(2) inarekebishwa kwa kufuta **"jadweli"** na kuweka badala yake maneno **"Jaweli La Pili" yaliopo baina ya neno "katika" na "la"** Aidha, marekebisho hayo yafanyike kila yanapojirejea maneno hayo ndani ya kanuni hizi yakitajwa fomu za ZPC.

18. Kanuni ya 18(3) inarekebishwa kwa kufuta maneno **"itatiwa sahihi"** na kuweka badala yake **"itawekwa saini".**

19. Kanuni ya 18(5) inarekebishwa kwa kufuta maneno **"mfanya kazi"** na kuweka badala yake neno **"mfanyakazi".**

20. Kanuni ya 19 inarekebishwa kwa kufuta maneno "**miezi sita**" na kuweka badala yake maneno **"mwaka mmoja".** 25(m)

21. Kanuni ya 26 (1) inarekebishwa kwa kufuta na kuandikwa upya kama ifuatavyo:

**“kutakuwa na muundo wa mshahara wa shirika ambao utaandaliwa na Mkurugenzi Mkuu na kuwasilishwa kwa Bodi kwa ajili ya kupendekezwa na kuwasilishwa Kamisheni ya Utumishi wa Umma kwa kuidhinishwa 25(o) PSA.**

Kanuni ya 26 (2) inarekebishwa kama ifuatavyo:

a) kwa kufuta maneno **“na kuuufanyia marekebisho madogo madogo”** na kuweka badala yake maneno **“na kuufanyia marekebisho ya**” baina ya neno **“kuupitia”** na **“muundo”.**

b) Kwa kututa neno **“waziri”** na kuweka badala yake maneno **“Mamlaka Husika”** 25(o)PSA

22. Kanuni ya 30 inarekebishwa kwa kufutwa na kuandikwa upya kama ifuatavyo:

**“kutakuwa na Muundo wa Utumishi katika Shirika utakaoandaliuwa na Mkurugenzi Mkuu na kupendekezwa na Bodi na kuidhinishwa na Kamisheni ya Utumishi wa Umma, ambao utaeleza nafasi zote katika Shirika pamoja na kuzingatia namna ya kupandisha vyeo wafanyakazi viwango vya nafasi na stahiki zao”.** 25(o) PSA.

23. Kanuni ya 31(5) inarekebishwa kwa kuingiza maneno ya **“kupendekeza kwa Bodi na Bodi itaidhinisha hatua za kuchukuwa”** baina ya neno **“hatua”** na **“ama”.**

24. Kanuni ya 36(3)(d) inarekebishwa kwa kufuta maneno **“miwili”** na kuweka badala yake **“mitatu”** (78(2)(i) kanuni ya utumishi (RPSA)).

25. Kanuni ya 37 inarekebishwa kwa kufutwa na kuandikwa upya kama ifuatavyo:

**“Shirika litawapatia viongozi wa Shirika vyombo vya usafiri kulingana na cheo cha mfanyakazi kama ilivyoelekezwa katika Muundo na Ngazi ya Utumishi wa Shirika na itakavyoamuliwa na Bodi”.**

26. Kanuni ya 40(2) inarekebishwa kwa kuifuta.

27. Kanuni ya 46(2) inarekebishwa kama ifuatavyo:

a) kufuta neno **“kukataa**” liliopo baina ya neno **“linaweza”** na “**kutoa”.**

b) kufuta maneno **“atashindwa kutoa**” liliopo baina ya neno “**mfanyakazi”** na **“sababu”** na kuweka badala yake neno **“atatoa”.**

28. Kanuni ya 48 inarekebishwa kama ifuatavyo:

Kwa kufuta maneno ya pembeni na kuandika upya na kusomeka:

**“posho la safari zinazogharamiwa na taasisi nyengine**”

29. Kanuni ya 55 inarekebishwa kwa kufuta maneno **“namb 2 ya 2011”** na kuweka badala yake maneno “**ya Zanzibar”.**

30. Kanuni ya 56(2) inarekebishwa kwa kufuta neno “**ataachishwa”** na badala yake **“kustaafishwa”.**

31. Kanuni ya 57 inarekebishwa kama ifuatavyo:

a) kufuta maneno ya pembeni na kuandika upya kama ifuatavyo: “utaratibu wa kustaafu kwa hiyari”

b) kanuni ndogo ya 1, inarekebishwa kwa:

i. kufuta maneno “wa miaka kumi na tano mfululizo” yaliopo baina ya neno **“muda”** na **“anaweza”** na kuweka badala yake maneno **“usiopungua miaka kumi na tano mfululizo na ametimia umri wa miaka hamsini na tano**”.

ii. kufuta maneno **“hata kama hajafikia umri wa kustaafu”** yaliopo baina ya neno **“hiari” na “baada”.**

32. Aidha, katika Kanuni ndogo ya 5, haiendani na maudhui ya kanuni hii na ilipaswa kuwekwa peke yake ambayo itazungumzia “**taarifa ya kuacha kazi**”.

33. Kanuni ya 58(1) inarekebishwa kwa kufuta neno **“atamuachisha”** kuweka badala maneno **“anaweza kumuachisha”** yaliopo baina ya neno **“mkuu”** na **“kazi”.**

34. Kanuni ya **58(2)** inarekebishwa kwa kufuta neno **“kustaafu”** kuweka badala yake neno **“kuachishwa”** yaliopo baina ya neno **“ya”** na **“atalipwa”.**

35. Kanuni ya 59(1) inarekebishwa kwa kufuta neno **"kukosa"** kuweka badala yake neno **"kosa"** yaliopo baina ya neno **"na"** na **"la".**

36. **Kanuni ya 60(2)** inarekebishwa kwa kufuta neno **"ni"** mwanzoni mwa kanuni ndogo ya (2)(a)(c)(d). pia inarekebishwa kwa kufuta neno "au" mwishoni mwa kanuni ndogo ya (2)(a)(b)(c).

37. **Kanuni ya 61(1)** inarekebishwa kwa kuingiza maneno **"la pili"** baina ya neno **"la" "kanuni".** Aidha, kufuta neno **"au"** katika aya ya (a).

38. Kanuni ya 62 inarekebishwa katika maneno ya pembeni kwa kuyafuta na kuyaandika upya na kusomeka kama ifuatavyo**: "uwanachama na michango katika mfuko wa hifadhi ya jamii"**

39. Kanuni ya **67(2)** inarekebishwa kwa kufuta **"60 (1) ya kanuni hii"** kuweka badala yake **"66 (1) ya kanuni hizi"**

40. Kanuni ya 69 inarekebishwa kwa kuongeza kanuni ndogo ya 6 kama ifuatavyo**:**

    **"Shirika linaweza kuanzisha daftari la mahudhurio la kielektroniki".**

41. Kanuni ya 70(1) inarekebishwa kwa kufuta **"60"** kuweka badala yake **"68" ya kanuni hizi"**

42. Aidha, katika kanuni ndogo ya (3) inarekebishwa kwa kufuta neno **"zida"** na kuweka badala yake neno **"ziada".**

43. Kanuni ya 77 inarekebishwa kwa kuingiza maneno **"lazima iombwe na mfanyakazi"** baina ya maneno **"malipo"** na **"na itaruhusiwa".**

44. Kanuni ya **83** inarekebishwa kwa kufuta maneno **"au ndugu yake wa kuzaliwa baba mmoja au mama mmoja"** yaliopo mwishoni mwa kanuni hiyo.

45. Kanuni ya **84(1) inarekebishwa** kwa kufuta neno **"kuchukuliwa"** kuweka badala yake neno **"kuchukuwa"** yaliopo baina ya neno **"anaweza" na "yote".**

46. Kanuni ya **85 i**narekebishwa kwa kufuta **"78"** kuweka badala yake **"84 ya kanuni hizi"**

    Aidha, kufutwa kwa maneno **"wa kiume"** yaliopo baina ya neno **"mfanyakazi"** na

**“atajifungua”** (economy of words and improper use of words)

47. Kanuni ya **88(3)** inarekebishwa kwa kufuta **“78”** kuweka badala yake **“89” ya kanuni hizi”**

48. Kanuni zinarekebishwa kwa kuingiza Kanuni mpya ya 95(1) itakayosomeka kama ifuatavyo

    Maneno ya Pembeni yawe **“kitambulisho cha kazi”**

49. Kanuni 95 husika itasomeka kama ifuatavyo:

    **a) 95(1) Shirika litatoa kitambulisho cha kazi kwa kila mfanyakazi;**

    **b) 95(1) ya awali kuwa 95(2) ambapo itasomeka kama kivyokuwa “Kila mfanyakazi anatakiwa kuvaa kitambulisho cha kazi wakati wote akiwa kazini”.**

    c) Aidha, Kanuni ya awali ya 95(2) inarekebishwa kuwa kanuni ya 96 na zilizobaki kufata mtiririko wa nambari hizo.

50. Kanuni ya 97 inarekebishwa kwa kuingiza maneno **“akipatikana na hatia”** baina ya neno **“na”** na **“atawajibika**”

51. Kanuni ya 100 inarekebishwa kwa kufuta neno **“kifungu”** na kuweka badala yake **“Kanuni”.**

52. Kanuni ya 103(2) inarekebishwa kwa kufuta neno **“wa”** liliopo baina ya neno **“wake”** na **“kumalizika”.**

**NAOMBA KUWASILISHA**

**RASIMU YA MAREKEBISHO YA KANUNI KWA HATUA ZAKO**

**Kiambatanisho No. 2**

## MAJUMUISHO YA KAMATI YA KANUNI NA SHERIA NDOGONDOGO KANUNI ZA MWENENDO WA MAHKAMA YA KADHI, 2021

**Maelezo ya Awali**

Kamati ilianza kuipitia Kanuni hii ya Mwenendo wa Mahakama ya Kadhi kuanzia tarehe 19/07/2022 hadi tunahitimisha leo kwa lengo la kufanya majumuisho. Katika kuipitia Kanuni hii, Kamati ililenga kuangalia yafuatayo:-

1. Misingi ya utungaji na uandishi wa sheria
2. Upeo (Scope) wa Kanuni kwa mujibu wa kifungu elekezi (enabling provision)
3. Lugha iliyotumika; na
4. Matumizi ya Kanuni hii.

Katika upitiaji wa Kanuni hii, Kamati iliweza kukutana na Makadhi wa Wilaya zote, Makadhi wa Rufaa, Mawakili pamoja na Mavakili kwa nyakati tofauti. Aidha, kamati imegundua yafuatayo;

**1. Ushirikishwaji wa Wadau**

Kamati imegundua kuwa Idadi kubwa ya wadau haikupata fursa ya kutoa maoni yao wakati wa utungaji wa Kanuni hii, na hata hao walishirikishwa mawazo yao hayakutiliwa maanani ipasavyo. Hali hii imepelekea baadhi ya matakwa ya Kanuni hii kutotekelezeka vile ambavyo *practice* ilivyo katika Mahakama zetu za Kadhi.

**Mfano:** Kanuni ya 101 imeshindwa kutoa nguvu za kuchukua hatua ipasavyo pale inapotokezea kudharauliwa kwa Mahakama.

Hivyo, tunashauri kupata maoni yakinifu kutoka kwa wadau husika ili Kanuni hii iweze kuendana na uhalisia wa Mahakama zetu za Kadhi

2. **Scope ya Kanuni**

Kanuni zipo vizuri na zimeratibu vyema uendeshaji wa mashauri katika Mahakama za Kadhi**. Aidha,** Kanuni hizi zimeakisi mwenendo mzima wa uendeshaji wa mashauri ya madai kuanzia uwasilishwaji wa hati za madai hadu utoaji wa hukumu kama ilivyoratibiwa chini ya Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Madai ya Zanzibar. Hata hivyo, kutokana na mapungufu yalimo katika Sheria, ikiwemo mahitaji ya Mahakama za Kadhi, jurisdiction ya mahakama hizi, vigezo vya maulamaa, mamlaka ya wasuluhishi na kadhalika umeondosha nguvu za Kanuni hizi.

3. **Matumizi ya lugha**

| SN | Hoja | Inavosomeka | Mapendekezo | Maoni |
|---|---|---|---|---|
| Kanuni ya 3 | Neno ‘**Mdaawa**’ au ‘**Wadaawa**’ | Maneno haya yametumika katika kanuni mbalimbali yakimaanisha Mdaiwa au Wadaiwa.<br><br>Hata hivyo hayakutolewa tafasiri ndani ya Kanuni hii. | Neno ‘Wadaawa’ kupatiwa tafsiri kama ilivyo katika Sheria.<br><br>Kufutwa kwa neno ‘Mdaawa’ | |
| Kanuni ya 6 | Mtiririko wa Kanuni | Kanuni ya 6,7,8 na 10 zinahusiana na maudhui ya hati za madai na majibu | Kanuni hizi zihamishiwe sehemu ya saba ambapo imebeba maudhui mazima ya HATI ZA | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | MADAI KWA UJUMLA | |
| Kanuni ya 8 | Mtiririko wa matumizi ya maneno.<br><br>'Ukanushaji'<br>'kukataa' | (2)Ukanushaji chini ya aya (a) ya kanuni ndogo ya (1) hautakuwa wa kukataa kiujumla lakini utapaswa kujibu hoja muhimu | Hivyo tunashauri isomeke:<br><br>'Ukanushaji chini ya aya (a) ya kanuni ndogo ya (1) hautakuwa wa kukanusha kiujumla lakini utapaswa kujibu hoja muhimu' | |
| Kanuni ya 9 | Sheria ya Mwenendo wa Kesi za Madai imeweka muda wa kuwasilishwa kwa majibu | Endapo mdaiwa atashindwa kuwasilisha majibu ya hati ya madai ndani ya muda uliopangwa na Mahkama, na Mahkama imejiridhisha kuwa hakuna sababu ya msingi, itaendendelea kusikiliza ushahidi wa upande mmoja na | Tunashauri isomeke;<br><br>Endapo ndani ya siku ishirini na moja (21) mdaiwa atashindwa kuwasilisha majibu ya hati ya madai, na Mahkama imejiridhisha kuwa hakuna sababu ya msingi, itaendendelea kusikiliza ushahidi | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | kutoa hukumu | wa upande mmoja na kutoa hukumu | |
| Kanuni ya 11 | Uainishwaji wa muda wa kuwasilisha utetezi wa madai ndani ya madai | Endapo mdaiwa yeyote ataibua madai ndani ya madai, mdai atapaswa kujibu madai ndani ya madai, na atayawasilisha Mahkamani na kwa mdaiwa majibu ya utetezi wa madai ndani ya madai katika muda ambao utaelekezwa na Mahkama. | Endapo mdaiwa yeyote ataibua madai ndani ya madai, mdai atapaswa kujibu madai ndani ya madai, na atayawasilisha Mahkamani si zaidi ya siku kumi na nne (14)na kwa mdaiwa majibu ya utetezi wa madai ndani ya madai yatawasilishwa Mahkama ndani ya siku kumi na nne (14) | |
| Kanuni ya 15 | Marekebisho ya neno | (2) Mtu **hatoeongezwa** kama ni mdai bila ya ridhaa yake ambayo ataithibitisha kwa maandishi au kwa namna nyengine itakayoidhinishwa | Tunashauri isomeke:<br><br>Mtu **hatoengezwa** kama ni mdai bila ya ridhaa yake ambayo ataithibitisha kwa maandishi au kwa | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | namna nyengine itakayoidhinishwa | |
| Kanuni ya 18(6) | Matumizi ya Neno Afisa | ……Endapo Afisa mpelekaji hati ya wito amewasilisha | Tunashauri kutumia neno Tarishi badala ya afisa kwa mujibu wa Sheria za Utumishi wa Umma | |
| Kanuni ya 25 | Kuweka matakwa ya sheria | (1) Kwa kuzingatia kifungu cha 19 cha Sheria, Mahkama inaweza kuamuru wadaawa kuhudhuria kwa msuluhishi kwa ajili ya hatua ya usuluhishi | Kwa kuzingatia kifungu cha 19 cha Sheria, Mahkama inaweza **ndani ya siku tano za kazi kuanzia tarehe ya kufunguliwa kesi**, kuamuru wadaawa kuhudhuria kwa msuluhishi kwa ajili ya hatua ya usuluhishi | |
| Kanuni ya 27 | Mgongano wa Sheria na Kanunu uteuzi wa Ulamaa | Kanuni ya 7.-(1) inasomeka<br><br>'Jaji Mkuu kwa kushauriana na Kadhi | Tunashauri kanuni kufuata matakwa ya sheria | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Mkuu atateua Ulamaa ambao …………<br><br>Kifungu cha 15(3) inasomeka<br><br>'Ulamaa watateuliwa na Mrajis wa Mahakama ya Kadhi…………' | | |
| Kanuni ya 35 | Kulegeza masharti | Mahkama inaweza katika hatua yoyote ya shauri kuamuru kutupiliwa mbali hati ya madai au majibu ya hati…………….. | Mahkama inaweza katika hatua yoyote ya shauri kuamuru kutupiliwa mbali **au kuelekeza vyenginevyo kwa** hati ya madai au majibu ya hati | |
| Kanuni ya 40 | Kutoeleweka maudhui yaliyokusudiwa | (1) Endapo hakuna **mdaawa** aliyehudhuria wakati shauri limepangwa kwa kusikilizwa, Mahkama inaweza | Kamati kupata ufafanuzi | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | kutoa amri ya kufuta shauri hilo | | |
| Kanuni 49 | Privacy ya uendeshaji mashauri | 49(1)……..litasikilizwa na kuamuliwa katika Mahkama ya wazi. | Tunashauri kuondosha ukwakasi kwa Makadhi ili kuweka privacy ya mashauri yao | |

**4. Ufafanuzi unaohitajika**

i. Kanuni hii imeratibu mwenendo wa mashauri kiujumla, ila je

   a. hatukuona haja ya kuweka sehemu mahsus katika Kanuni hii zinayoweka mienendo ya mashauri yanayohusiana na ndoa na talaka, mirathi au usimamizi wa watoto?

   b. fatwa zinazohusina na hiba, amana za kidini na misaada zinaratibiwaje ndani ya Kanuni hii ukizingatia kuwa ni miongoni mwa kazi za Mahakama kwa mujibu wa Kifungu cha 5(d) cha sheria?

ii. Kwa mujibu wa kifungu cha 6 cha Sheria ya Kadhi, ushahidi utakuwa kwa mujibu wa Kanuni na Sheria za Kiislamu tu, utaratibu uliotumika katika Kanuni ya 50 ni wa Sheria au Kanuni ipi?

iii. Je kwanini kanuni ya 26 isitoe pia mamlaka ya kutengua uteuzi wa Wasuluhishi?

iv. Je ni utaratibu upi utatumika kulipia gharama za magereza pale mdaiwa atakapoamriwa kwenda chuo cha mafunzo chini ya kanuni ya 119

## 5. Maoni ya Jumla

Kamati inapongeza jitihada kubwa iliyofanyika kupatikana kwa Kanuni ya kwanza katika uendeshaji wa Mahakama zetu za Kadhi, hata hivyo tunashauri yafuatayo;

1. Kufanyiwa maboresho kwa haraka katika maeneo tuliyoainisha na mengineyo
2. Kutungwa kwa kanuni za adhabu kwa mujibu wa sheria za Kiislamu
3. Kufanyiwa maboresho sheria ya Mahakama ya Kadhi, 2017 ili kuipa ufanisi mzuri Mahakama zetu

Mwisho tunashukuru Uongozi wa Wizara akiwemo Naibu Katibu Mkuu, Naibu Kadhi, Kaimu Mrajis wa Mahkama Kuu kwa mashirikiano makubwa waliyoipa Kamati yetu kwa takriban wiki nzima sasa na tunategemea mabadiliko yatapatikana kwa haraka.

**Kiambatanisho No. 3**

## MAONI YA KAMATI
## KANUNI ZA UTUMISHI ZA SHIRIKA, 2021

5. **Hoja za jumla**

- Makosa ya kiuandishi katika kanuni hii kuna makosa ya aina hayo ambayo yanahitajikuazingatiwa wakati wa kuandika maandishi ya kisheria kwani katika kanuni hiii haikuzingatia umoja na wingi (singular means plural) hivyo kamti inaagiza uandishi wa kanuni uzingatie suala hilo.

- Suala la uandishi wa nambari ndani ya kanuni umejitokeza katika kanuni nyingi kama 77(1),59(1),89(1), 91(1)(3),124(2), 134 hivyo kamati inashauri kuziweka katika hali ya maandishi.

- Katika kanuni ya 81(2) kamati inahitaji ufaafanuzi wa kina nini inamaanisha kanuni hiyo.

- Kanuni ya 84 kumejitokeza neno moja kutumika tofauti ka **“angestahili”** na **“angestahiki”.**

- Kanuni ya 86 kimejirejea kinafanana na kanuni ya 81.

- Kanuni ya 90 kamati inashauri kuangaliwa upya kulingana na sheria ya utumishi wa umma.

- Katika kanuni ya 102(d)(e) ni aya ambazo hazihusiani na dhana ya kanuni hiyo ya usalama wa sehemu za kazi.

- Kanuni ya 111 aya ya (f)na (k) zimejirejea kwani zipo katika kanuni ya 106 na 104(c).

- Kanuni ya 115(3) kamati inataka kufahamu kwa nini adhabu inatolewa na kamati ya nidhamu na isitolewe na mamlaka ya nidhamu.

- Kanuni ya 151 dhana yake imejirejea katika kanuni ya 138 hivyo ifutwe moja.

- Kanuni ya 116(5) kulingana nasheria ya utumishi wa umma ikiwa mfanyakazi ameadhibiwa kwa adhabu ya kifungo kisichopungua miezi sita jela ndio atapewa adahbu ya kufukuzwa kazi.

- Kanuni ya 119 imeelezea kuhusu makosa makubwa ya nayompelekea mfanyakazi huyo kwa mujibu wa kanuni ya 117 kufukuzwa kazi papo hapo kamati ianshauri kuangaliwa upya adhabu hiyo kwani inaenda kinyume na sheria ya utumishi wa umma namb.2/2011 katika jadweli la kwanza la A la kosa la kwanza ambayo linataka mfanyakazi huyo kuonywa kwa mdomo na sio kufukuzwa kazi.

- Kanuni ya 112(2) pia imeweka adhabu ambayo kiuhalisia inatolewa na mahakama nayo ni faini.

6. **Hoja Mahsus**

| No. | Hoja | Inavosomeka | Mapendekezo | Maoni |
|---|---|---|---|---|
| Kanuni ya 5 | Kubadilisha na kufuta maneno<br><br>i. Watendaji na kuweka wafanyakazi<br><br>ii. Kuondosha neno kutekeleza | (2) Mkurugenzi Mkuu atawajibika kusimamia utendaji kazi wa Shirika na atasimamia **watendaji** wote watakaoajiriwa na Shirika na kutekeleza kazi nyengine yoyote atakayoagizwa na Bodi **kutekeleza** | Mkurugenzi Mkuu atawajibika kusimamia utendaji kazi wa Shirika na atasimamia wafanyakazi wote watakaoajiriwa na Shirika na kutekeleza kazi nyengine yoyote atakayoagizwa na Bodi | |
| Kanuni ya 6 | Utaratibu mzuri wa uandishi | (2) Kamati Tendaji itajumuisha wajumbe wafuatao:<br><br>(a) Mkurugenzi Mkuu ambaye atakuwa Mwenyekiti;<br><br>(b) Mkurugenzi Idara ya Utumishi na uendeshaji; (c) Mkurugenzi Idara ya Ufundi;<br><br>(d) Mkurugenzi Idara ya Habari na Matukio;<br><br>(e) Mkurugenzi Idara ya Uzalishaji wa Vipindi; (f) Mkurugenzi Idara ya Masoko;<br><br>(g) Mkuu Afisi ya Mratibu Pemba; | (2) Kamati Tendaji itajumuisha wajumbe wafuatao:<br><br>(a) Mkurugenzi Mkuu ambaye atakuwa Mwenyekiti;<br><br>(b) Wakurugenzi wa Idara;<br><br>(c) Mkuu Afisi ya Mratibu Pemba;<br><br>(d) Wakuu wa Vitengo;<br><br>(e) Mwanasheria; na | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | (h) Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi;<br><br>(i) Mkuu wa Kitengo cha Fedha;<br><br>(j) Mkuu wa Kitengo cha Tehama;<br><br>(k) Mkuu wa Kitengo cha Mipango;<br><br>(l) Mwanasheria; na<br><br>(m) Wakuu wa maeneo mengine kwa mujibu wa muundo<br><br>kama ulivyowekwa na Shirika. | (f) Wakuu wa maeneo mengine kwa mujibu wa muundo kama ulivyowekwa na Shirika | |
| Kanuni ya 7 | Kubadilisha maneno na kurekebisha aya | Kamati Tendaji itakuwa na **Kamati** zifuatazo: | 7. Kamati Tendaji itakuwa na kazi zifuatazo: | |
| | | b) kuandaa sera na mipango ya utekelezaji wa kazi za Shirika; | b)Kuandaa mpango wa utekelezaji kazi wa shirika na kuuwasilisha katika bodi kwa kuidhinishwa; | |
| | | d) kuhakikisha kuwa uongozi wa Shirika unafuata Sheria na kanuni zilizopo katika hatua zote | Kufuta Aya ya (d) kwani ni miongoni mwa majukumu ya bodi | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Kanuni ya 8 | Kuondosha maneno | (1) Kamati tendaji itakutana angalau mara moja kwa kila mwezi au wakati wowote **itakapoona** itakapotokea hali ya dharura | 8.-(1) Kamati tendaji itakutana angalau mara moja kwa kila mwezi au wakati wowote itakapotokea hali ya dharura | |
| | kanuni ndogo ya (2) kuongeza neno **“wa”** baina ya neno **“wajumbe”** na **“kamati”.** | (2) Zaidi ya nusu ya idadi ya wajumbe Kamati Tendaji watatosha kufanya akidi ya kikao | (2) Zaidi ya nusu ya idadi ya wajumbe **wa** Kamati Tendaji watatosha kufanya akidi ya kikao | |
| Kanuni ya 9 | kuongeza maneno | (2)(c) Mwanasheria; | c) Mwanasheria wa Shirika; | |
| | | (2)(d) Wajumbe wengine wasiozidi watatu watakaoteuliwa na Mkurugenzi Mkuu; na | (2)(d) Wajumbe wengine wasiozidi watatu **ambao ni wafanya kazi wa shirika** watakaoteuliwa na Mkurugenzi Mkuu; na | |
| | | (3) Mhasibu Mkuu wa Shirika atakuwa ni Katibu<br><br>(4) Mkurugenzi Mkuu wakati atakapoteua Wajumbe wa Kamati ya Nidhamu chini ya kanuni ndogo ya (2) (e) ya kanuni hii atazingatia jinsia. | **(3) afisa utumishi wa shirika atakuwa katibu**<br><br>(4) Mkurugenzi Mkuu wakati atakapoteua Wajumbe wa Kamati ya Nidhamu chini ya kanuni ndogo ya **(2) (d)** ya kanuni hii atazingatia jinsia. | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Kanuni ya 10 | Kubadilisha maneno | (d) kuhakikisha kuwa matatizo ya wafanyakazi wanapatiwa ufumbuzi unaostahili; | (d) kuhakikisha kuwa matatizo ya wafanyakazi wanapatiwa ufumbuzi **unaostahiki**; | |
| | | (f)kuhakikisha wafanyakazi wanatekeleza sheria na kanuni za wafanyakazi muda wote; | (f) **kuhakikisha wafanyakazi wanafuata sheria, kanuni na miongozo yote ya shirika**; | |
| Kanuni ya 12 | Kufuta maneno | 4). Kwa madhumuni ya kanuni hii, vyeo **vya juu na vya chini** vya wafanyakazi katika Shirika vitatofautishwa kulingana na nafasi na ngazi ya mshahara kama itakavyoelezwa katika Muundo wa Utumishi **utakaoandaliwa na** Shirika chini ya kanuni ya 32 ya Kanuni hizi. | 4). Kwa madhumuni ya kanuni hii, vyeo vya wafanyakazi katika Shirika vitatofautishwa kulingana na nafasi na ngazi ya mshahara kama itakavyoelezwa katika Muundo wa Utumishi wa Shirika chini ya kanuni ya 32 ya Kanuni hizi. | |
| Kanuni ya 13 | Kubadili maneno | a) ni **Mtanzania**, isipokuwa kama aina ya ajira itaruhusu kuajiriwa raia wa kigeni; | a) ni Mzanzibari, isipokuwa kama aina ya ajira itaruhusu kuajiriwa raia wa kigeni; | |
| Kanuni ya 16 | Kufuta kanuni na kuandika upya | (1)Wafanyakazi wanapotaka kufikiriwa kwa nafasi za kazi zote zinazoweza kutokea kazini wakati wakiwa hawapo kazini kwa muda mfupi kwa sababu ya ugonjwa au likizo lazima wafanye | (1) Wafanyakazi wanapotaka kufikiriwa kwa nafasi za kazi zote zinazoweza kutokea kazini wakati wakiwa hawapo kazini kwa muda mfupi kwa sababu ya ugonjwa au likizo, wakuu wa idara | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | mipango na wakuu wa Idara zao ili waarifiwe juu ya nafasi zinazoweza kutokea wakati wao watakapokuwa hawapo kazini. | watatakiwa kuwapa taarifa juu ya nafasi zilizowazi na utaratibu wa kujaza nafasi hizo | |
| Kanuni ya 17 | Kubadilisha aya | c) Wakurugenzi wa Idara | (c)Mkurugenzi wa utumishi na uendeshaji | |
| Kanuni ya 19 | Kufuta kanuni ndogo ya (1) na (2) na kuandika upya | (1) Mfanyakazi aliyeajiriwa na Shirika atajaza mkataba wa ajira kama ulivyoelezwa katika Jadweli la Pili la Kanuni hizi, ili kuonesha utayari wake wa kufanyakazi kwa bidii na uaminifu katika Shirika na kufuata masharti yote ya ajira.<br>(2) Mara baada ya kujaza mkataba wa ajira, Mfanyakazi atatakiwa kuweka saini yake katika sehemu inayomuhusu, na kwa upande wa Shirika, mkataba utatiwa saini na Mkurugenzi Mkuu. | (1)Mfanyakazi aliye ajiriwa na shirika atajaza mkataba wa ajira kama ulivyoelezwa katika jadweli la pili la kanuni hizi na atatakiwa kuweka saini yake sehemu inayomuhusu na kwa upande wa shirika mkataba utawekwa saini na Mkurugenzi Mkuu | |
| Kanuni ya 24 | | 3) Kabla ya uajiri wa mfanyakazi kufutwa kwa mujibu wa masharti ya kanuni ndogo ya (2) ya kanuni | 3) Kabla ya uajiri wa mfanyakazi kufutwa kwa mujibu wa masharti ya kanuni ndogo ya (2) ya kanuni | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | hii, mamlaka husika itamtaka mfanyakazi huyo kujieleza ndani ya saa 72 sababu zilizomfanya kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo, na endapo mfanyakazi atatoa maelezo yasiyoridhisha uteuzi wake utafutwa<br><br>(4) Baada ya **uteuzi wa** mfanyakazi kufutwa, mamlaka husika itamjulisha kwa maandishi mfanyakazi huyo juu ya uamuzi wa kufutwa **kazi**. | hii, mamlaka husika itamtaka mfanyakazi huyo kujieleza ndani ya saa 72 sababu zilizomfanya kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo, na endapo mfanyakazi atatoa maelezo yasiyoridhisha ajira yake itafutwa<br><br>(4) Baada ya ajira ya mfanyakazi kufutwa, mamlaka husika itamjulisha kwa maandishi mfanyakazi huyo juu ya uamuzi wa kufutwa ajira yake. | |
| Kanuni ya 26 | Kuongeza maneno | (4) Bila ya kujali masharti ya kanuni ndogo ya (2) ya kanuni hii, mfanyakazi aliye katika kipindi cha majaribio anaweza kufutwa kazini ikiwa atafanya kosa kubwa la kinidhamu ambalo adhabu yake ni kufukuzwa kazi. | (4) Bila ya kujali masharti ya kanuni ndogo ya (2) ya kanuni hii, mfanyakazi aliye katika kipindi cha majaribio anaweza kufutwa kazini ikiwa atafanya kosa kubwa la kinidhamu ambalo adhabu yake ni kufukuzwa kazi kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma | |
| Kanuni ya 45 | Kufutwa kwa kanuni ndogo ya (2) na (3) | (2) Kwa madhumuni ya kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii, Shirika halitoruhusu mfanyakazi kuchukua mkopo mpaka mfanyakazi atakapoweka dhamana | Zimefutwa | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | inayolingana na kiwango cha mkopo.<br><br>(3) Bila ya kuathiri masharti ya kanuni hii, Shirika linaweza kuandaa mkataba baina yake na mfanyakazi anayetaka kukopa, kwa ajili ya kuweka masharti ya kuonesha namna gani mfanyakazi anaweza kulifidia Shirika pale itakapotokea hali itakayopelekea kushindwa kulipa deni alilokopa. | | |
| Kanuni ya 60 | Kuifuta kanuni na kuiandika upya | (1) Ikiwa Mkurugenzi Mkuu ataona mfanyakazi hatekelezi kikamilifu kazi zake alizopangiwa kwa sababu ya maradhi, ataiomba Bodi ya Madaktari imfanyie uchunguzi kama afya yake inamruhusu kuendelea na utumishi au kustaafishwa ikiwa afya yake haimruhusu kuendelea na kazi.<br><br>(2) Mfanyakazi ambaye ataachishwa kazi kwa sababu ya maradhi atapewa mshahara wa miezi mitatu baada ya taarifa pamoja na mafao ya kiinua mgongo na pencheni | Ikiwa Mkurugenzi Mkuu ataona mfanyakazi hatekelezi kikamilifu kazi zake alizopangiwa kwa sababu ya maradhi, ataiomba Bodi kutoa ridhaa ya kuchunguzwa afya ya mfanyakazi huyo kupitia Bodi ya Madaktari na endapo ikithibitisha afya ya mfanayakazi huyo haimruhusu kuendelea na kazi taratibu kisheria za utumishi zitafuatwa. | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa. | | |

**Kiambatanisho No. 4**

**YALIYOBAINIKA NA KAMATI YA KANUNI NA SHERIA NDOGO NDOGO KATIKA UCHAMBUZI WA KANUNI ZA UTUMISHI ZA MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE ZANZIBAR,2016**

**ZINAZOTOLEWA NA MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE**

| UK | MAPUNGUFU | INAYOSOMEKA SASA | MAPENDEKEZO YA KAMATI | MAJIBU YA WIZARA |
|---|---|---|---|---|
| 727 | Sehemu ya Kwanza<br><br>Kanuni ya 3 (UFAFANUZI) | *(a)* **“Bodi”** | katika utaratibu wa uandishi neno **“Bodi”** liwe mwanzo kufanyiwa tafsiri badala ya neno **“Bodi ya Ukaguzi wa Afya”** | |
| | | *(b)* **“Bodi ya Ukaguzi wa Afya” ………………………………..** | **neno “Bodi ya Ukaguzi wa Afya” maana yake haiku vyema inashauriwa kuandika chini ya Sheria gani na kifungu gani cha Sheria hiyo** | |
| | | *(c)* **“Daktari aliyethibitishwa” ……………………………………………..** | **neno “Daktari aliyethibitishwa”** hakuna neno hilo katika sheria namba12 ya mwaka 1999, bali kuna neno **“Daktari”**<br><br>maneno **“Kamati Tendaji”**<br><br>maneno **“mkurugenzi wa vitendo”** kufutwa badala yake kuandikwa maneno **“Wakuu wa Idara”** | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | ***(d)*** **"Kamati Tendaji"** | maana ya neno hilo kuangaliwa na kuandikwa upya kwani kosa lake kama la Kamati Tendaji | |
| | | ***(e)*** **"Menejimenti"** | maneno **"Kanuni za Maadili**" maana yake imetafsiriwa ni kanuni zinazotokana na kanuni hizi. Kimsingi sio sawa kisheria Kanuni kuzaa Kanuni **"deligation cannot deligaro"** | |
| | | ***(f)*** **"Kanuni ya Maadili"** | maana yake ni kitengo cha utekelezaji wa shughuli za Mamlaka<br><br>(pia Kamati inahitaji ufafanuzi zaidi) | |
| | | ***(g)*** **"Kitengo"** | Ifanyiwe tafsiri kwa mujibu wa sheria ya dawa za kulevya<br><br>Kamati inahitaji ufafanuzi zaidi | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | **“Madawa ya kulevya”**<br><br>**Mkurugenzi**<br><br>**Mtegemezi**<br><br>**Mlezi**<br><br>**Rushwa**<br><br>**Udanganyifu**<br><br>**Uhamisho** | Kamati inahitaji ufafanuzi zaidi<br><br>Kamati inahitaji ufafanuzi zaidi<br><br>Ifanyiwe tafsiri kwa mujibu wa Sheria ya Rushwa<br><br>Ifanyiwe tafsiri kwa mujibu wa Sheria ya Jinai<br><br>Kamati inahitaji ufafanuzi zaidi kwani tafsiri haiku sawa | |
| 686 | Sehemu ya pili<br><br>Kanuni ya 4 | Kanuni ya 4(1) na (2) | inarekebishwa kufuta neno “**utakaopitishwa**” liliopo baina na neno *“***na”** na ***“na”*** **na** kuweka badala yake **“utakaopendelezwa”**<br><br>kwa mujibu wa kf 25(0) cha Sheria namba 2 ya 2011. Aidha marekebisho | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | hayo pia yafanyike katika **kf 4(2)** | |
| | Kanuni ya 5 | | **Hakuna muunganiko wa kanuni ya 5(3) na(4) na maudhui ya kanuni hii** | |
| 687 | Kanuni ya 6<br><br>Na kanuni ya 7 | Kanuni ya 6 na ya 7 zinarekebishwa<br><br>Kwa kufuta neno **“majukumu”** na kuweka badala yake neno **“wajibu”** | **Kamati inataka kufahamu tofauti baina ya neno kazi, wajibu na majukumu** | |
| | Kanuni ya 10 na 11 | Kanuni ya 10 ,11 na 16 zinarekebishwa<br><br>Kwa kufuta | **Kamati imeona kwamba hazina mantiki** | |
| | Kanuni ya 41 | Kanuni ya 41 inafanyiwe marekebisho kwa kufuta maneo “isiyozidi miaka mitatu”. | **Kamati imeona kuwa zipo kozi ambazo zinazidi muda wa miaka mitatu.Mf. Shahada ya Uhandisi na Sheria.** | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Kanuni ya 43 | Ifanyiwe marekebisho kwa kuongoza maneno ‘**kupitia kwa Mkuu wa Idara**” mwisho wa kanuni hiyo.<br><br>Kanuni ya 43 (2) na (3) zifutwe . | **Kamati inaona ni vyema mkuu wa Idara awe na taarifa ya ombi la likizo ya mtumishi aliye chini yake.**<br><br>**Kamati imeona kuwa vifungu hivyo vimewekwa vyama katika Kanuni ya Utumishi wa Umma.** | |
| | Kanuni ya 47 | Kanuni ya 47(2) inarekebishwa kwa kufuta maneno **“kwa lazima”**<br><br>Kanuni ya 47(3) inarekebishwa kwa kufuta neno **“maamlumu”** na kuweka badala yake neno **“maalumu”** | **Kamati imeona ni vyema kuondoa mameno hayo ili kuweza kujumuisha mazingira yote ya kustaafu. iwe kwa hiari au lazima.** | |
| | Kanuni ya 48 | Kanuni ya 48 inarekebishwa kwa kuongeza mananeo **“nje ya kituo chake cha kazi”** baina ya maneno “**ndani ya Tanzania**” na **“atakuwa”** | **Kamati imeona posho la kujikimu utaratibu wake ni kwa mtumishi anayesafiri nje ya kituo cha kazi tu.** | |
| | Kanuni ya 50 | Ifanyiwe marekebisho kwa;<br>• Kufuta 50(1).<br>• Kuhamisha Kanuni ya 50(2) kuwa 47(3) | **Ipo sawa na Kanuni ya 47(1)**<br><br>**Maudhui yake yanaendana na Kanuni hiyo hivyo ni vyema kuwekwa hapo.** | |
| | Kanuni ya 56 | Kanuni ya 56 inarekebishwa | Kamati imezingatia Kanuni | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | kwa kufuta na kuandikwa upya kama ifuatavyo:<br><br>**“Posho la Samani linaweza kulipwa na Mamlaka kwa Mkurugenzi Mkuu kila baada ya miaka mitano kwa idhini ya Bodi”** | ya Utumishi wa Umma Kanuni ya 127 na hivyo kuwaondoa wale wote ambao hawana nyazifa za uteuzi wa Rais.<br><br>Mkurugenzi Mkuu analingana hadhi ya Makatibu Wakuu. | |

**MAKOSA NA MAONI YA JUMLA KATIKA KANUNI ZA UTUMISHI ZA MAMLAKA YA VIWANJA VYA NDEGE ZANZIBAR, 2016**

i. Kwamba hakuna muunganiko wa Kanuni ya 5(3) na (4) na maudhui ya kanuni hii

ii. Kanuni ya 6 imetoa majukumu ya muajiri Kamati ilitaka kufahamu muajiri ni nani. Aidha, Kanuni zilipaswa kubainisha kwa kutafsiri, kuanzisha au kuainisha kutoka kwenye Sheria.

iii. Kanuni ya 11(3) Kamati inataka kufahamu kwamba Kanuni hiyo inaendena na matakwa ya Sheria za Utumishi.

iv. Kanuni ya 11(2) na Kanuni 12(d) Kamati inataka kujua ni nani haswa anatoa matokeo ya usajili ……Je ni bodi au Mamlaka.

v. Ni nani anaendesha mafuzo kwa mujibu wa Kanuni ya 17 ……. Neno mwajiri limetumika kwa chombo gani ……Bodi au Mamlaka.

vi. Mamlaka ya kufanya uhamisho wa Mtumishi iwe ya Mkurugenzi Mkuu na sio ya Mkurugenzi wa Idara………. Kanuni ya 21.

vii. Kanuni ya 32(3) kinyume na utaratibu wa sasa wa utumishi hakuna limbikizo la likizo.

viii. Kanuni ya 34(2) kawaida siku za likizo huhesabika siki za kazi na sio za mwisho wa wiki au siku za mapunziko.

ix. Kanuni ya 37(2) ipo vyema

x. Manemo ya pembeni hayaendani na maudhui ya kanuni 47(2) na kuendelea.

xi. Kanuni ya 63. Kamati inahitaji ufafanuzi juu ya uwepo wa Sera husika na ipo chini ya Taasisi gani.

xii. Kanuni ya 66(4) Kamati inahitaji ufafanuzi Zaidi, kwani Kanuni ya Utumishi wa Umma imeelekeza kwa mtumishi aliye likizo na anasafiri nje ya nchi anatakiwa kutoa taarifa tu kwa mkuu wake wa Kazi na haikueleza kuwa atakosa fursa za matibabu.

xiii. Kanuni ya 76(a) na (d) zinaongea kitu kimoja.

xiv. Kanuni ya 77(e) Kamati inataka kufahamu utaratibu ukoje pamoja na kuonesha muda kwa malipo hayo katika Kanuni ya 77(a).

xv. Kanuni ya 80……. sio sahihi kwa Kanuni kutoa Mamlaka ya kutungwa Kanuni nyengine. Hivyo kamati inataka kufahamu uwezo huo umetokana na Kifungu gani cha Sheria.

xvi. Kanuni ya 89. Kinafutwa.Zipo sheria zinazosimamia ujinai wa masuala haya kwa mtu yeyote. Hivyo hakuna mantiki ya kuweka kifungu hicho ktk Kanuni hii.

xvii. Kanuni ya 90. Siku 7 ni Kidogo sana kwa kumpa mtu fursa ya kukata rufaa. Kawaida ya Sheria nyingi ni siku 30 zikiwemo Sheria ya Mwenendo wa jinai na Madai.Kwani dhamira ni kutoa haki kwa asiyeridhika na wakati mwengine huhitaji ushauri wa kitaalamu kwa mtu mwengine,hivyo siku 7 ni chache mno.

Naomba kuwasilisha.

**Kiambatanisho No. 5**

**MAPENDEKEZO YA MAREKEBISHO YA KAMATI YA KANUNI NA SHERIA NDOGO YA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU KANUNI ZA UTUMISHI ZA SHIRIKA, 2021**

1. Kanuni ya 3 kinarekebishwa katika neno "UONGOZI" na kuandika upya kama ifuatavyo:

**"maana yake ni uongozi wa shirika unaojumuisha wakurugenzi wa idara, wakuu wa vitengo pamoja na wakuu wa divisheni: na"**

2. Kanuni ya 5 kinarekebishwa kama ifuatavyo:
   a) kufuta neno **"watendaji"** na kuweka badala yake neno "**wafanyakazi".**
   b) kufuta neno **"kutekeleza"** liliopo mwishoni mwa kanuni hiyo.

3. Kanuni ya 6(2) inarekebishwa kwa kufuta ya (h) (i) (j) (k) (l) (m) na kuweka badala yake aya nyengine kama ifuatavyo:
   a) Aya (h) Wakuu wote wa idara
   b) Aya (i) Wakuu wote wa vitengo: na
   c) Aya (j) Mwanasheria.

4. Kanuni ya 7 inarekebishwa kama ifuatavyo:
   a) kufutwa neno **"kamati"** liyopo baina ya neno **"na"** na **"zifuatazo"** na kuweka badala yake neno **"kazi".**
   b) Katika aya ya (a) kufuta na kuandika upya kama ifuatavyo **"kuandaa taarifa za utekelezaji kazi kwa kila robo mwaka na kuwasilisha katika bodi".**
   c) Katika aya (b), kufuta na kuandika upya kama ifuatavyo.

   **"Kuandaa sera na mipango ya utekelezaji kazi wa shirika na kuwasilisha katika bodi kwa kuidhinishwa"**

   d) Kufuta Aya ya (d) kwani ni miongoni mwa majukumu ya bodi.

5. Kanuni ya 8 inarekebishwa kama ifuatavyo:
   a) kanuni ndogo ya (1) kufuta neno **"itakapoona"** liliopo baina ya neno **"wowote"** na **"itakapotokea"**

   b) kanuni ndogo ya (2) kuongeza neno **"na"** baina ya neno **"wajumbe"** na **"kamati".**

6. Kanuni ya 9 inarekebishwa kama ifuatavyo:
   a) kanuni ndogo (2) katika aya ya zifuatazo;

i. aya (b), kufuta na kuandika upya aya hiyo kwa sasa itasomeka " mkuu wa idara yoyote ya shirika.
ii. aya (c), kuongeza maneno "wa shirika" mwishoni mwa aya hiyo.
iii. Aya (d), Kwa kuongeza maneno "**ambao ni wafanya kazi wa shirika"** baina ya neno **"watatu"** na **"watakaoteuliwa"**

b) kanuni ndogo (3) kwa kufuta na kuandika upya na kusomeka **"afisa wa utumishi wa shirika atakuwa katibu wa kamati ya nidhamu".**

c) kanuni ndogo (4) kamati inashauri kufutwa maneno kanuni ndogo ya(2)(e) na kuweka badala yake Kanuni ndogo ya(2)(d) ama kam,ati inahitaji ufafanuni wa wizara nini wamekusudia.

7. Kanuni ya 10 inarekebishwa kama ifuatavyo:
   a) katika aya (d), kufuta neno **"unaostahili" na** kuweka badala yake neno **"unaostahiki".**

   b) katika aya (e), kufuta maneno **"yanaboreshwa mara kwa mara"** na kuweka badala yake neno **"yanaimarishwa"**

   c) katika aya (f), kufuta aya hiyo na kuandika upya **"kuhakikisha wafanyakazi wanafuata sheria, kanuni na miongozo yote ya shirika".**

   d) katika aya ya (g), kufuta neno **"nasaha"** yaliopo baina ya neno **"ushauri" na "wafanyakazi".**

8. Kanuni ya 12 inarekebishwa kama ifuatavyo:
   a) kanuni ndogo (3), kufutwa neno "kuathiri" na kuweka badala yake neno "kujali".

   b) kanuni ndogo (4), inarekebishwa kama ifuatavyo:
      i. kufuta neno "vya juu na chini" yaliopo katika mstari wa kwanza wa kanuni ndogo hiyo.
      ii. kufuta neno **"itakavyoelezwa"** na kuweka badala yake neno "**ilivyoelekezwa**".
      iii. kufuta maneno **"utakaoandaliwa na"** na kuweka badala yake neno **"wa".**

9. Kanuni ya 13 inarekebishwa kwa kufuta neno "**Mtanzania"** na kuweka badala yake neno **"mzanzibar".**

10. Kanuni ya 15 inarekebishwa kwa:
    a) kwa kufuta neno "**mwaminifu"** na kuweka badala yake neno **"muaminifu".**
    b) kwa kufuta maneno "**utovu wa nidhamu"** na kuweka badala yake neno **"kinidhamu".**

11. Kanuni ya 16 inarekebishwa kama ifuatavyo:
    a) kanuni ndogo ya (1) kufuta na kuandika upya kama ifuatavyo:
    "wafanyakazi wanapotaka kufikiriwa kwa nafasi za kazi zote zinazoweza kutokea kazini wakati wakiwa hawapo kazini kwa muda mfupi kwa sababu ya ugonjwa au likizo lazima wakuu wa idara wawape taarifa juu ya nafasi zilizowazi na utaratibu wa kujaza nafasi hizo".

    b) kanuni ndogo ya (2) inarekebishwa kama ifuatavyo:
        (i) kufutwa maneno **"hawapo kazini kwa muda mrefu au wapo"** yaliopo mwishoni mwa mstari wa kwanza wa kanuni ndogo hiyo na kuweka badala yake neno "watakuwa.
        (ii) kufutwa maneno **"kabla ya kuondaka"** yaliopo mwanzoni mwa mstari wa tatu wa kanuni ndogo hiyo.

12. Kanuni ya 17 inarekebishwa kama ifuatavyo:
    a) kanuni ndogo ya (2) inarekebishwa kama ifuatavyo:
        (i) kwanza kamati ya ajira ni kubwa
        (ii) aya (b) kwa kufuta neno **"wasiopongua"** na kuweka badala yake neno **"wasiozidi"**
        (iii) aya (c) kwa kufuta neno **"wakurugenzi wa idara"** na kuweka badala yake maneno **"Mkurugenzi wa rasilimali watu"**
        (iv) aya (e) kufuta na kuwa 'proviso'.

    b) kanuni ndogo ya (3) inarekebishwa kuongeza maneno **"itamualika mkuu wa idara husika na"**.

    c) kanuni ndogo ya (5) inarekebishwa kufuta neno "**au"** na kuweka badala neno **"na".**

13. Kanuni ya 19(1)(2)inarekebishwa kwa kufutwa na kuandika upya kama ifuatavyo "**mfanayakazi aliye ajiriwa na shirika atajaza mkataba wa ajira kama ulivyoelezwa katika jadweli la pili la kanuni hizi na atatakiwa kuweka saini yake sehemu inayomuhusu na kwa upande wa shirika mkataba utawekwa saini na mkurugenzi mkuu"**

14. Kanuni ya 20 inarekebishwa kwa kufuta neno "kwa" na kuweka badala yake neno "na".

15. Kanuni ya 22 inarekebishwa kama ifutavyo:
    a) kanuni ndogo ya (1) inarekebishwa kama ifuatavyo:
        i) aya ya (a) kwa kufuta maneno **"kwa madhumuni ya kanuni hii umri wa kustaafu kwa lazima kwa mujibu wa sheria inayotumika Zanzibar"** na kuweka badala yake neno "**au kwa njia nyengine yoyote kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma Zanzibar**".

ii) Aya ya (b) kwa kufuta neno **“itaelekezwa”** na kuweka badala yake neno **“imeelenzwa”.**

b) kanuni ndogo ya (2) inarekebishwa kwa kufuta maneno “**kwa vipindi**” na kuweka badala yake maneno “**miwili kwa vipindi visivyozidi**”.

c) kanuni ndogo ya (3) inarekebishwa kwa kufuta maneno “**yule wa ajira ya**” na kuweka badala yake neno **“wa”.**

d) kanuni ndogo ya (4) inarekebishwa kwa kufuta maneno “**atatakiwa kufanya kazi kwa bidi na ujuzi na uwezo wakena kufuata masharti yote ya ajira kama mfanyakazi wa kawaida**” na kuweka badala yake maneno **“kufuata masharti ya utumishi wa umma”.**

16. Kanuni ya 24 inarekebishwa kama ifuatavyo:
    a) kanuni ndogo ya (3) inarekebishwa kwa kufuta maneno “**uteuzi wake utafutwa**” na kuweka badala yake maneno “**ajira yake itafutwa”.**

    b) Kanuni ndogo ya (4) inarekebishwa kwa:
        i. kufuta maneno “**uteuzi wa**” na kuweka badala yake maneno “**ajira ya”.**
        ii. kufuta neno “**kazi**” na kuweka badala yake maneno “**uajiri wake”.**

17. Kanuni ya 25 inarekebishwa kwa kufuta maneno **“kazini kwa mfanyakazi huyo”** na kuweka badala yake neno **“kazi”.**

18. Kanuni ya 26 inarekebishwa kama ifuatavyo:
    a) kanuni ndogo ya (1) inarekebishwa kwa kufuta maneno **“kazini mfanyakazi huyo”** na kuweka badala yake neno **“kazi”.**

    b) kanuni ndogo ya (4) inarekebishwa kwa:
        i. kufuta neno **“kazini”** na kuweka badala yake neno **“kazi.**

        ii. Kuongeza maneno**“kwa mujibu wa sheria ya utumishi wa umma”.**

19. Kanuni ya 29(2) inarekebishwa kwa kuongeza neno **“kuu”** mwishoni mwa kanuni ndogo hiyo.

20. Kanuni ya 31(4)(d) inarekebishwa kwa kuongeza maneno **“au makato mengine yoyote kwa mujibu wa sheria”** mwishoni mwa aya hiyo.

21. Kanuni ya 33 inarekebishwa kwa kuongeza maneno **“kwa mujibu wa masharti ya sheria ya utumishi wa umma”** mwishoni mwa kanuni hiyo.

22. Kanuni ya 36(3) inarekebishwa kwa kuongeza neno **“saba”** mwishoni mwa kanuni hiyo.

23. Kanuni ya 44 inarekebishwa kwa kufuta neno **“jili”** liliopo baina ya neno **“kwa”** na **“ya”** kanuni hiyo na kuweka badala yake neno **“ajili”.**

24. Kanuni ya 45 inarekebishwa kwa kufuta kanuni ndogo ya (2) na (3).

NOTE (…… **kwani dhamana ya mkopo wa mfanyakazi ni mshahara wake kwa muajiriwa wake).**

25. Kanuni ya 48 inarekebishwa kama ifuatavyo:

a) Kanuni ndogo ya (1) Kuongeza maneno **“kwa kuzingatia toleo la maafa la utumishi wa Serikali Kuu”** mwishoni mwa kanuni ndogo hiyo. Aidha, Kamati inataka kufahamu kama toleo hilo lipo ili kuona kama kifungi hiki kitakuwa kinaweza kufanya kazi.

b) Kanuni ndogo ya (2) kufutwa.

26. Kanuni ya 53 inarekebishwa kwa kufuta neno **“zake”** yaliopo baina ya neno **“saa”** na **“za”.**

27. Kanuni ya 54 inarekebishwa kwa kufuta neno **“mtumishi”** na kuweka badala yake neno **“mfanyakazi”.**

28. Kanuni ya 58 inarekebishwa kwa kufuta maneno **“kila mwaka meneja ”** yaliopo mwanzoni mwa kanuni hiyo na kuweka badala yake maneno **“mkurugenzi wa”.**

29. Kanuni ya 59 inarekebishwa kwa kufuta maneno **“kipindi kisichozidi miaka miwili”** yaliopo mwishoni mwa kanuni hiyo na kuweka badala yake maneno kwa kuzingatia masharti ya sheria ya utumishi wa umma.

30. Kanuni ya 60 inarekebishwa kwa kufuta na kuandikwa upya kama ifuatavyo: **“*ikiwa mkurugenzi mkuu ataona mfanyakazi hatekelezi kikamilifu kazi zake alizopangiwa kwa sababu ya***

***maradhi, ataiomba bodi kutoa ridhaa ya kuchunguzwa afya ya mfanyakazi huyo kupitia bodi ya madaktari na endapo bodi hiyo ikithibitisha afya ya mfanayakazi huyo haimruhusu kuendelea na kazi taratibu kisheria za utumishi zitakuatwa".***

31. Kanuni ya 65(3) inarekebishwa kwa kufuta neno **"na"** yaliopo baina ya neno **"kosa"** na **"wizi"** na kuweka badala yake **"la".**

32. kanuni ya 72(1) inarekebishwa kwa kufuta neno **"jaduweli"** yaliopo baina ya neno **"katika"** na **"la"** na kuweka badala yake neno **"jadweli"**.

33. Kanuni ya 73 inarekebishwa kwa kufuta neno **"wafanyakazi wote wa shirika"** yaliopo mwanzoni mwa kanuni hiyo na kuweka badala yake maneno "**mfanyakazi wa shirika anatakiwa**".

34. Kanuni ya 77(2 inarekebishwa kwa kufuta maneno **"wakurugenzi wa idara watawajibika"** yaliopo mwanzoni mwa kanuni hiyo na kuweka badala yake "**mkurugenzi wa idara ya rasilimali watu atawajibika".**

35. Kanuni ya 83(2) inarekebishwa kwa kuingiza maneno **" baada kupata idhini ya bodi"** yaliopo baina ya neno **"itaruhusiwa"** na **"ikiwa".**

36. Kanuni ya 89 inarekebishwa kwa kufuta neno **"mine"** yaliopo baina ya neno **"miezi"** na **"na"** na kuweka badala yake neno **"minne".**

37. Kanuni ya 91 inarekebishwa kwa kufuta neno **"atakojifungua"** yaliopo baina ya neno **"kike"** na **"atapewa"** na kuweka badala yake neno **"aliyejifungua".**

38. Kanuni ya 94(2) inarekebishwa kwa kufuta maneno **"ilambayo"** yaliopo baina ya neno **"kama"** na **"itaitumia"** na kuweka badala yake maneno **"ile ambayo".**

39. Kanuni ya 101 inarekebishwa kwa kufuta neno **"naatawajibika"** yaliopo baina ya neno **"kinidhamu"** na **"kupewa"** na kuweka badala yake maneno **"na ikithibiti atawajibika".**

40. Kanuni ya 104 inarekebishwa kama ifuatavyo:

i. kwa kuingiza neno **"na ikithibiti"** baina ya neno **"na"** na **"atawajibika".**
ii. aya ya (c) kwa kufuta maneno **"kama hati halali"** yaliopo mwishini mwa aya hiyo.

41. Kanuni ya 105 inarekebishwa kwa kuingiza neno **“ikithibiti”** baina ya neno **“na”** na **“atawajibika”.**

42. Kanuni ya 106 inarekebishwa kwa kuingiza neno **“ikithibiti”** baina ya neno **“na”** na **“atawajibika”.**

43. Kanuni ya 107 inarekebishwa kama ifuatavyo:

a) kanuni ndogo ya (1) kwa kuingiza neno **“ikithibiti”** baina ya neno **“na”** na **“atawajibika”. Aidha uandishi huo unahitajika katika kanuni ya 108(4), 109, 110 iwe kama proviso ya kanuni ya 111“akipatikana na hatia”** maneno hayo yatumike**.**

b) kanuni ndogo ya (2) kwa kufuta maneno **“na ukimwi na au virusi vya ukimwi na”** yaliopo baina ya neno **“na”** na **“mfanyakazi”.**

44. Kanuni ya 110 inarekebishwa kwa kufuta neno **“hzii”** liliopo mwishoni na kuweka badala yake neno **“hizi”.**

45. Kanuni ya 113 inarekebishwa kwa kufuta kanuni ndogo ya (1) na kuandika upya kama ifuatavyo “**Bila ya kuathiri masharti ya jumla ya kanuni hizi utaratibu wa hatua za kinidhamu utakuwa kama ulivyoelezwa na sheria nam.2 ya 2011**”.

46. Kanuni ya 117 inarekebishwa kwa kufuta maneno **“ya ajira na”** na kuweka badala yake maneno **“ya utumishi wa umma”.**

47. Kanuni ya 133(2) inarekebishwa kwa kufuta neno “**hazitotolewa”** na kuweka badala yake neno **“hazitatolewa**”.

48. Kanuni ya 138 iarekebishwa katika maneno yake ya pembeni kwa kufuta na kuandika upya kama ifuatavyo **“madeni ya mfanyakazi wa shirika”.**

## MAONI YA JUMLA YA KAMATI

- Makosa ya kiuandishi : Katika kanuni hii kuna makosa ya aina hayo ambayo yanahitaji kuzingatiwa wakati wa kuandika maandishi ya kisheria kwani katika kanuni hiii haikuzingatia

umoja na wingi (singular means plural) hivyo Kamati inaagiza uandishi wa kanuni uzingatie suala hilo.

- Suala la uandishi wa nambari ndani ya kanuni umejitokeza katika kanuni nyingi kama 77(1), 59(1), 89(1), 91(1)(3), 124(2), 134 hivyo kamati inashauri kuziweka katika hali ya maandishi.

- Katika kanuni ya 81(2) kamati inahitaji ufafanuzi wa kina nini inamaanisha kanuni hiyo.

- Kanuni ya 84 kumejitokeza maneno mawili kutumika kwa dhana moja ambapo huo si utaratibu wa uandishi **"angestahili"** na **"angestahiki".**

- Kanuni ya 86 imejirejea inafanana na kanuni ya 81.

- Kanuni ya 90 kamati inashauri kuangaliwa upya kulingana na Sheria ya Utumishi ya Umma.

- Katika kanuni ya 102(d)(e) ni aya ambazo hazihusiani na dhana ya kanuni hiyo ya usalama wa sehemu za kazi.

- Kanuni ya 111 aya ya (f)na (k) zimejirejea kwani zipo katika kanuni ya 106 na 104(c).

- Kanuni ya 115(3) kamati inataka kufahamu kwa nini adhabu inatolewa na kamati ya nidhamu na isitolewe na mamlaka ya nidhamu.

- Kanuni ya 151 dhana yake imejirejea katika kanuni ya 138 hivyo ifutwe moja.

- Kanuni ya 116(5) kulingana nasheria ya utumishi wa umma ikiwa mfanyakazi ameadhibiwa kwa adhabu ya kifungo kisichopungua miezi sita jela ndio atapewa adahbu ya kufukuzwa kazi.

- Kanuni ya 119 imeelezea kuhusu makosa makubwa ya nayompelekea mfanyakazi huyo kwa mujibu wa kanuni ya 117 kufukuzwa kazi papo hapo kamati ianshauri kuangaliwa upya adhabu hiyo kwani inaenda kinyume na sheria ya utumishi wa umma namb.2/2011 katika jadweli la kwanza la A la kosa la kwanza ambayo linataka mfanyakazi huyo kuonywa kwa mdomo na sio kufukuzwa kazi.

- Kanuni ya 112(2) pia imeweka adhabu ambayo kiuhalisia inatolewa na mahakama nayo ni faini.

- Kanuni ya 7 kazi za kamati tendaji ziangaliwe upya kwani kazi nyengine ni kazi za bodi kwa mujibu wa sheria
- Kanuni ya 6 kamati tendaji haijajumuisha uongozi wa shirika kwa upande wa afisi ya Tanzania bara.

- Kanuni ya 8 iundwe upya kwa kufanya kanuni mbili tofauti hivyo suala la akidi ya kikao liwekewe kanuni yake. Pia marekebisho hayo yafanywe katika kanuni ya 1.

- Kanuni ya 9 aya ya d, ichanganywe na kanuni ya 9(4) pia jukumu la muhasibu alilokasimiwa katika 9(3) apewe mwanasheria.

- Kanuni ambazo kamati inapendekeza zifutwe nazoni:
    a) 10(e),(g)…..

- Kanuni 12 suala la ajira libakie kwa bodi kwani kwa mujibu wa sheria ya shirika bodi ndio msimamizi mkuu wa watumishi wa shirika pia sheria ya utumishi inazitambua bodi kama mamlaka za ajira…………………………….

- Masharti ya kanuni ya 13 yanapingana na sheria ya utumishi ni vyema sheria ya utumishi ikazingatiwa.

- Kamati ya ajira ni kubwa sana ni vyema ikapunguzwa.

- Aidha kamati inashauri maudhui ya kanuni 11 hadi 22 yaangaliwe upya.

- Kamati inataka kufahamu katika Kanuni ya 27 ni nani mwenye mamlaka ya uhamisho wa wafanyakazi ieleze.

- Kanuni ya 29 kamati inakubaliana na mantiki na maudhui ya kifungu hicho hata hivyo uandishi haujakaa vyema.

- Kamati inashauri katika kanuni ya 34 kwamba kanuni za sheria ya utumishi zizingatiwe kwani hakuna muda wa majaribio katika suala la upandishwaji wa cheo isipokuwa kuna dhana ya kukaimu kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma.
- Kanuni ya 44 inayohusu mkopo wa wafanyakazi kamati inataka kufahamu dhana ya shirika kutoa mkopo kwa wafanyakazi aidha inapendekeza kianuni hiyo ifutwe.

- Kamati inapenekeza kufutwa kwa Kanuni ya 48 kwani suala lolote la maafa linaratibiwa na mamlaka nyengine kisheria.

- Katika kanuni ya 51 kamati inataka kufahamu utekelezaji wa kanuni hiyo iwapo hautaleta changamoto yoyote.

- Kanuni ya 55 kamati inataka kufahamu utekelezaji wa kanuni hii ukoje (utaratibu wake).

- Kanuni ya 57 kamati inashauri kanuni hiyo izungumzie "mazingira magumu' na sio "bidhaa chafu"

- Kanuni 65 kamati inashauri utaratibu wa kushughulikia makosa kwa wafanyakazi ufuate utaratibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma.

- Kamati inashauri kanuni ya 74,75 na 76 zifutwe kwani sheria ya utumishi kifungu 65 kimeshazungumzia suala hilo.

- Kanuni ya 103 ifutwe ushauri wa kamati.

- Kanuni ya 104(d)(e) kamati inahitaji ufafanuzi kwani haieleweki dhana ya aya hizo.

- Kanuni ya 111 aya ya (f) na (k) zimejitokeza katika kanuni nyengine hivyo zifutwe.

- Kanuni ya 116(b) maneno sheria ya kazi yafutwe na kuwekwa badala yake Sheria ya Utumishi wa Umma. (kwa mujibu wa sheria ya utumishi wa umma kifungu 2. Inaweka wazi kwamba Sheria ya Utumishiwa Umma ni kiongozi )

- Kanuni ya 121 iweke wazi suala ya rufaa iwapo mfanyakazi hakuridhika na uamuzi wa bodi je rufaa yake itakwenda katika mamlaka gani.

- Kanuni ya 122 kamati inataka kufahamu suala la fedha za mafuzo kwa wafanyakazi wa shirika je zinatengwa katika bajeti.

- Kanuni ya 125 kufutwa maneno "kwa nia safi"

- Kanuni ya 127 na 128 ziunganishwe kwani zinazungumzia dhana moja.

- Kanuni ya 133,134,135,136,137,138,139,140,142,147,148149 na 151 zifutwe

- Kwa ujumla kanuni ilitarajiwa kuzungumzia mambo ya msingi ya uendeshaji wa shirika la utangazaji hata hivyo inaonekana imejikita Zaidi katika kuzungumzia masuala ya kiutumishi ambayo yameshazungumzwa kwa kina na sheria ya utumishi na kanuni zake. Hivyo kifanya kanuni hii kuwa ni marejeo ya kanuni ya utumishi kamati inashauri kuzingatiwa yaliobainika katika kanuni hiyo.